JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2021

## ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2021

# 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

*Kimechapishwa na*:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es salaam, Tanzania

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021**

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

DIBAJI .... iv
1.0 UTANGULIZI .... 1
2.0 UCHAMBUZI WA KILA SWALI .... 2
2.1 Sehemu A: Majibu ya Kuchagua na Kuoanisha. .... 2
2.1.1 Swali la 1: Sunnah na Hadithi .... 3
2.1.2 Swali la 2: Tawhiid .... 12
2.2 Sehemu B: Majibu Mafupi .... 17
2.2.1 Swali la 3: Tawhiid .... 17
2.2.2 Swali la 4: Tarekh .... 22
2.2.3 Swali la 5: Qur’an .... 30
2.3 Sehemu C: Majibu Mafupi na Insha .... 33
2.3.1 Swali la 6: Fiqh kwa Ujumla .... 33
2.3.2 Swali la 7: Fiqh ya Swala. .... 48
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA .... 53
4.0 HITIMISHO .... 54
5.0 MAPENDEKEZO .... 54
KIAMBATISHO .... 55

## DIBAJI

Taarifa hii ya uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) 2021 somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu inatoa mrejesho kwa wadau kuhusu ufaulu wa wanafunzi katika upimaji wa somo hili na kubainisha sababu mbalimbali zilizochangia katika ufaulu huo.

Uchambuzi uliofanywa katika taarifa hii umebainisha sababu zilizochangia matokeo ya wanafunzi katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu FTNA 2021. Uchambuzi umebainisha wanafunzi waliopata alama za juu, wastani na za chini katika kila swali. Aidha, sampuli za majibu ya wanafunzi waliofanya vizuri na wale waliofanya vibaya zimeoneshwa. Sababu zilizowafanya baadhi ya wanafunzi kuweza kujibu maswali kwa usahihi ni pamoja na kuwa na ufahamu wa kutosha juu ya mada zilizopimwa na kuelewa matakwa ya maswali yaliyoulizwa. Aidha, uchambuzi huu umebaini kuwa baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu maswali kwa usahihi hawakuwa na ujuzi wa kutosha katika mada mbalimbali za Elimu ya Dini ya Kiislamu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya maswali.

Baraza la Mitihani lina imani kuwa, mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau wote wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji hatimaye kuondoa changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii. Endapo mapendekezo yaliyotolewa mwishoni mwa taarifa hii yatazingatiwa, ni imani ya Baraza kuwa kiwango cha kufaulu katika somo hili kitaongezeka.

Baraza la Mitihani linatoa shukrani za dhati kwa wote waliohusika katika uandishi wa taarifa hii.



Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inawasilisha matokeo ya uchambuzi wa kina wa majibu ya wanafunzi waliofanya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) mwezi Novemba mwaka 2021 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Upimaji huu uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo husika uliotolewa mwaka 2012 kwa kidato cha I na II.

Maswali yaliyotumika katika upimaji yaliandaliwa kutoka katika fani tano ambazo ni: *Sunna na Hadithi, Tawhiid, Historia (Tarekh), Qur'an na Fiqh*. Maswali hayo yaligawanywa katika sehemu tatu; A, B na C zenye jumla ya alama 100. Sehemu A ilikuwa na maswali mawili (1 na 2), sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3, 4 na 5) na mwisho sehemu C ilikuwa na maswali mawili (6 na 7). Mwanafunzi alitakiwa kujibu maswali yote katika vipengele vyote.

Wanafunzi waliosajiliwa kufanya upimaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2021 walikuwa 92,021. Kati yao wanafunzi 85565 sawa na asilimia 92.98 walifanya upimaji. Idadi hii inaonesha ongezeko la wanafunzi 3,233 ikilinganishwa na wanafunzi 82,332 waliofanya upimaji wa somo hili mwaka 2020. Kati ya wanafunzi 85,565 waliofanya upimaji mwaka huu 2021, wanafunzi 34,260 (40.23%) walifaulu katika madaraja mbalimbali. Jedwali lifuatalo linaonesha madaraja ya wanafunzi hao ikilinganishwa na mwaka 2020.

**Jedwali Na. 1: Ulinganifu wa Ufaulu Kati ya Mwaka 2020 na 2021**

| **Mwaka** | **% ya Ufaulu** | **Madaraja** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | A | B | C | D | F |
| 2020 | 65.94 | 314 | 1,527 | 16,334 | 36,054 | 28,006 |
| 2021 | 40.23 | 147 | 675 | 8,154 | 25,284 | 50,897 |

Jedwali linaonesha kushuka kwa kiwango cha ufaulu kwa asilimia 25.71 ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo wanafunzi walifaulu kwa asilimia 65.94.

Taarifa hii imechambua majibu ya wanafunzi katika kila swali kwa kulinganisha na matakwa ya swali husika na majibu yake na kile ambacho wanafunzi wamejibu na kufafanua majibu hayo. Aidha, sampuli za majibu sahihi na yasiyo sahihi ya wanafunzi zimeambatanishwa kwa lengo la

kuonesha namna wanafunzi wanavyopaswa kujibu maswali. Taarifa hii imebainisha changamoto zilizowakabili wanafunzi katika kujibu maswali kiusahihi ili zifanyiwe kazi. Pamoja na uchambuzi wa majibu ya wanafunzi, taarifa hii imebainisha ufaulu wa wanafunzi katika mada mbalimbali zilizopimwa. Madaraja ya ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu yalikuwa kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 2: Madaraja ya Ufaulu Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu**

| Alama | Daraja | Maoni |
|---|---|---|
| 75 - 100 | A | Vizuri Zaidi |
| 65 - 74 | B | Vizuru Sana |
| 45 - 64 | C | Vizuri |
| 30 - 44 | D | Inaridhisha |
| 0 - 29 | F | Dhaifu |

Jedwali la madaraja ya ufaulu linaonesha kuwa daraja la juu la ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni A na daraja la mwisho ni F. Pamoja na kuwa madaraja matano ya ufaulu kama yalivyooneshwa kwenye jedwali, taarifa hii itatumia madaraja matatu katika kuwasilisha ngazi za ufaulu ambayo ni: vizuri, wastani na dhaifu. Ufaulu ulikuwa dhaifu kama asilimia ya wanafunzi waliofanya vizuri ni 0 hadi 29. Ufaulu ulikuwa wa wastani ikiwa waliofaulu swali ni kati ya asilimia 30 hadi 64 na ufaulu ni mzuri ikiwa ni asilimia 65 hadi 100

Hitimisho na mapendekezo kutokana na uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umetolewa katika sehemu ya mwisho ya taarifa hii. Matokeo ya uchambuzi huu yanatarajia kutumika katika kuimarisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Elimu ya Dini ya kiislamu kwa wanafunzi na hatimaye kuboresha kiwango cha ufaulu katika upimaji ujao.

## 2.0 UCHAMBUZI WA KILA SWALI


### 2.1 Sehemu A: Majibu ya Kuchagua na Kuoanisha.

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ambapo mwanafunzi alipaswa kujibu maswali yote. Swali la kwanza lilikuwa la kuchagua jibu sahihi katika vipengele kumi (i – x). Swali la pili lilikuwa la kuoanisha, ambalo pia lilikuwa na vipengele kumi (i – x). Kila swali lilikuwa na jumla ya alama kumi (10), alama moja (01) kwa kila kipengele hivyo sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 20.

### 2.1.1 Swali la 1: Sunnah na Hadithi

Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo manne aliyopewa (A, B, C na D) kisha kuandika jibu hilo katika kisanduku. Swali lilitoka katika mada ndogo za; *Maana na umuhimu wa Sunna na Hadithi, Mafunzo mbalimbali ya Hadithi zilizochaguliwa pamoja na uandishi na uchambuzi wa Hadithi za Mtume (S.A.W).*

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi wote 85,565 (100%) waliofanya upimaji huu, ambapo kati yao wanafunzi 53,315 (62.31%) walipata alama 3 hadi 6 ambazo ni alama za wastani. Wanafunzi 30,337 (35.48%) walipata alama 0 hadi 2 ambazo ni ufaulu dhaifu. Aidha, wanafunzi 1893 (2.2%) walipata alama kuanzia 7 hadi 10 ambazo ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao umeoneshwa katika Chati Na. 1.




**Chati Na. 1**. *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 1*.

Chati Na. 1 inaonesha kulikuwa na ufaulu wa wastani katika swali hili kwakuwa asilimia 64.52 ya wanafunzi wote walijibu kwa usahihi, ikilinganishwa na asilimia 35.48 ya wanafunzi waliopata ufaulu hafifu.

Aidha, wanafunzi waliopata alama za wastani walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Sunnah na Hadithi na kuelewa vema matakwa ya kila kipengele. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika kila kipengele ni kama ifuatavyo:

Katika kipengele cha (i) mwanafunzi alitakiwa kuonesha njia ambayo itawasaidia Waislamu kuweza kutofautisha Hadithi sahihi na Hadithi za uongo. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima wanafunzi umahiri wa kuchambua Hadithi ili kubaini usahihi wake. Wanafunzi mahiri katika dhana ya uchambuzi wa Hadithi waliweza kujibu kwa usahihi na kuchagua jibu sahihi B *kusisitizwa ufundishwaji wa somo la sayansi ya Hadith.* Wanafunzi hawa waliashiria kuelewa vema nafasi ya sayansi ya Hadithi katika kuchuja Hadithi na habari mbalimbali zinazohitaji ithibati. Aidha, wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki walionesha kukosa maarifa ya kutosha ya uchambuzi wa Hadithi kwani vipotoshi vyote walivyochagua (A, C na D) havibainishi sifa za Hadithi sahihi ambazo ni msingi wa kutofautisha baina yake na Hadithi za uongo.

Aidha, waliochagua kipotoshi D *kuwahimiza kusoma historia ya kuzuka hadithi za uongo,* walionesha kutoelewa vizuri matakwa ya swali kwani historia hiyo, inabainisha chanzo cha Hadithi hizo na makusudio au dhamira za kutungwa kwa Hadithi hizo. Wengine walichagua kipotoshi A *kuwahimiza waislamu kuhifadhi hadithi za Mtume (SAW).* Hoja hii haijibu swali kwa kuwa kama mtu hana maarifa ya kujua usahihi wa Hadithi anaweza kuhifadhi hata za uongo bila yeye kujua. Waliochagua kipotoshi C *Kuzingatia wanazuoni na vitendo vya maswahaba* walishindwa kuzingatia kuwa Uislamu hautegemei maoni tu ya watu au hadhi ya mtu kupima usahihi wa mambo kwani hata baadhi ya Hadithi hizo za uongo zilizushwa wakati wa maswahaba kutokana na migogoro baina yao.

Kipengele cha (ii) mwanafunzi alitakiwa kutofautisha kati ya Sunna na Hadithi. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima wanafunzi umahiri wa kuchambua dhana ya Sunna na Hadithi, ambapo wanafunzi waliokuwa na ufahamu wa kutosha juu ya dhana hiyo waliweza kuonesha tofauti kwa kuchagua jibu C *Sunnah ni vitendo na Hadithi ni nadharia* kwani Hadithi ni maelezo juu ya Sunna (Mwenendo) wa Mtume (SAW). Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili hawakuwa na maarifa juu ya dhana ya Sunna na Hadithi kwakuwa majibu yao yote hayakuwa na msingi wa kutofautisha baina ya dhana hizo.

Wanafunzi waliochagua herufi A *Sunnah zipo chache na Hadithi ni nyingi* walionesha kutojua uhusiano baina ya dhana hizo kwani haiwezekani kuwa

na maelezo ya vitendo ambavyo havijafanyika hivyo Hadithi haziwezi kuzidi idadi ya Sunna. Zaidi katika kipotoshi A ni kuwa hakuna kumbukumbu ya idadi baina ya Sunna na simulizi zake. Wanafunzi wengine walichagua kipotoshi B *Hadithi ni vitendo na Sunna ni nadharia* hawa walionesha kutokuwa na maarifa kabisa juu ya dhana hizo kwani hata maana ya maneno hayo (kama ilivyotolewa awali) haiwiani na uhusiano uliowekwa katika kipotoshi hicho. Aidha, waliochagua kipotoshi D *Hadithi ni lazima kuifuata na Sunna ni hiyari* walichanganya dhana ya Hadithi na Qur'an, kwani Qur'an ndio lazima kufuatwa maelekezo yake yote katika hali yoyote.

Katika kipengele cha (iii), mwanafunzi alitakiwa kubaini dhana ya Sunna kivitendo kwa kubainisha kitendo halisi kinachogusa maisha ya mtu anayefuata Sunna. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima wanafunzi umahiri wa kutumia Sunna katika maisha yake ya kila siku. Wanafunzi mahiri katika dhana ya Sunna waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki kwa kuchagua jibu B *kuwapenda jamaa zako*. Jambo hili limebainishwa na Mtume (SAW) kwa msisitizo wa maneno na vitendo kama lilivyoelezwa katika Hadithi mbalimbali k.v *"Anayehitaji kukunjuliwa katika rizki yake na aunganishe udugu"* (Bukhari na Muslim). Aidha, wanafunzi walioshindwa kuchagua jibu sahihi katika kipengele hiki walionesha kuwa na mitazamo isiyosahihi (misconceptions) katika vitendo vya Sunna kama ambavyo vinatambulishwa katika jamii.

Vipotoshi vyote katika kipengele hiki (A *Kuonja chakula kidogo,* C *Kuuza dawa za kiarabu* na D *Kuvaa kanzu siku zote*) vilihusu vitendo maarufu vinavyofanywa katika jamii na kunasibishwa na Sunna kwa mazoea hali ya kuwa havina uhusiano na dhana halisi ya Sunna.

Kipengele cha (iv) mwanafunzi alitakiwa kubaini idadi ya Hadithi zilizochini ya tanzu ya umaarufu. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima wanafunzi umahiri wa kukumbuka tanzu mbalimbali za Hadithi kama zilivyogawanywa katika sayansi ya Hadithi. Wanafunzi mahiri katika uchambuzi wa Hadith za mtume (s.a.w) waliweza kujibu kwa usahihi kwa kuchagua herufi A *Mbili* kwani chini ya tanzu hiyo kuna Hadithi Mutawatir na Hadithi Ahad. Aidha, wanafunzi waliochagua vipotoshi katika kipengele hiki walishindwa kukumbuka vema mgawanyo wa Hadithi katika tanzu

zake mbalimbali hivyo baadhi yao walijibu kwa kukosa maarifa na wengine kuchanganya na tanzu nyingine zinazoshabihiana.

Waliochagua kipotoshi B *Nne* walichanganya kigezo cha usahihi dhidi ya kigezo cha umaarufu hivyo wakashindwa kubaini kuwa halikuwa jibu sahihi na waliochagua kipotoshi C *Tatu* walishindwa kutofautisha kati ya aina za Hadithi na sehemu kuu za Hadithi ambazo ni Isnad, matini na Rawi. Kadhalika, wanafunzi waliochagua kipotoshi D *Tano* walichanganya mafunzo ya Hadithi juu ya nguzo tano za Uislamu na dhana ya Hadithi maarufu kwa kuwa nguzo za Uislamu ni maarufu.

Kipengele cha (v) mwanafunzi alitakiwa kutambua sifa ya mtu mwenye nguvu kwa mujibu wa mafundisho ya Mtume (SAW). Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima wanafunzi umahiri wa kuchambua mafunzo ya Hadithi mbalimbali alizojifunza darasani. Wanafunzi mahiri katika uchambuzi wa Hadithi waliweza kujibu kwa usahihi na kuchagua herufi D *Mwenye subira wakati wa hasira,* kwa kuwa hivyo ndivyo alivyomueleza Mtume (SAW) mtu mwenye nguvu kwa mtazamo wa Uislamu. Wanafunzi walioshindwa katika kipengele hiki baadhi yao hawakuwa na maarifa juu ya Hadithi hiyo ya Mtume (SAW) na wengine walichanganya mafundisho hayo na Hadithi zingine zinazosisitiza ubora wa Muislamu kuwa madhubuti kimwili na ile inayoeleza ubora au faida za ibada ya Funga.

Aidha, waliochagua kipotoshi A *Mwenye kudumu na ibada ya funga,* walichanganya mafunzo ya Hadithi na kurejea Hadithi nyingine ya Mtume (SAW) inayohimiza kufunga ili watu wapate afya. Hata hivyo, Hadithi hiyo haikuwa mahususi kubainisha sifa ya mtu mwenye nguvu kama lilivyotaka swali. Wengine walichanganya mafunzo ya Hadithi na kuchagua herufi B *Mwenye uwezo wa kupigana Jihadi.* Wanafunzi hawa walihusisha jibu hili na Hadithi nyingine ya Mtume (SAW) inayosema “Muislamu mwenye nguvu ni bora na anapendeza zaidi mbele ya Mwenyezi-Mungu kuliko Muislamu dhaifu (goigoi).” Pamoja na usahihi wa Hadithi hiyo lakini bado haijibu swali husika kwani Hadithi hiyo inaeleza ubora wa Muislamu kuwa madhubuti kimwili na haifafanui sifa ya mtu mwenye nguvu. Kundi lingine lililoshindwa kipengele hiki ni lile lililochagua herufi C *Mwenye kuvumilia wakati wa shida*. Hawa walihusisha jibu hili na uzoefu wa kijamii inapotokea mtu kuwa na uwezo wa kustahamili shida za kimaisha. Hili

halikuwa sahihi kwa sababu muktadha wa Hadithi hiyo haikukusudiwa nguvu za utafutaji katika maisha kuwa sifa hizo.

Kipengele cha (vi), mwanafunzi alitakiwa kubaini jina la kazi kubwa ya uandishi wa Hadithi iliyoonekana katika kipindi cha Maswahaba. Kipengele hiki kilipima umahiri wa mwanafunzi kukumbuka matukio muhimu katika Historia ya uandishi wa Hadithi. Wanafunzi walioweza kukumbuka vema historia ya uandishi wa Hadithi walijibu kwa usahihi na kuchagua herufi A *Al qatadaya.*

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi walionesha kuwa dhaifu katika historia ya uandishi wa Hadithi hivyo walichagua majibu yao kwa kudhania. Aidha, baadhi ya wanafunzi walioshindwa kipengele hiki walichagua kipotoshi B *Al Muwatta*, kwa sababu ya kutokujua historia ya kitabu hicho ambacho kiliandikwa wakati wa Tabiin, hivyo halikuwa jibu sahihi. Wengine  waliochagua vipotoshi C *Sahihi Bukhari* na D *Sahihi Muslim* hawakuwa sahihi kwa kuwa vitabu hivyo vyote viliandikwa kipindi cha *Tabii tabiina* na si katika kipindi cha Maswahaba.

Kipengele cha (vii), mwanafunzi alitakiwa kubaini moja ya tukio lililoonesha umuhimu wa kuhifadhiwa Hadithi mapema baada ya kufariki Mtume (SAW). Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima wanafunzi umahiri wa kuchambua matukio muhimu katika historia ya uandishi wa Hadithi ambayo yalisababisha haja ya kuandikwa kwa Hadithi kwa ujumla. Wanafunzi weledi wa historia ya uandishi wa hadithi za Mtume (SAW) walijibu kipengele hiki kwa usahihi na kuchagua herufi B *Sehemu ya kuzikwa Mtume (SAW)*, kwani mara baada ya Mtume (SAW) kufariki hoja ya sehemu ya kuzikiwa iliibuka hivyo kabla watu kupishana, mgogoro ule ukasuluhishwa kwa kumbukumbu ya Hadithi ambayo baadhi ya waliohudhuria waliiwasilisha kwa wenzao.

Aidha, matukio mengine yote yaliyotajwa katika vipotoshi (A *Kuibuka kwa Mitume wa uongo*, C *Usimamizi wa familia ya Mtume (SAW)* na D *Kuhamishwa kwa makao makuu ya dola ya Kiislamu*) pamoja na kuwa na mchango katika historia ya kuhifadhiwa kwa Hadithi hayakutosha kuwa sahihi kwa kuwa yalijitokeza baada ya Mtume (SAW) kuzikwa.

Kipengele cha (viii), mwanafunzi alitakiwa kubaini sifa kubwa ya Hadithi inayoitofautisha na Qur'an. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima wanafunzi umahiri wa kuelewa dhana ya Hadithi ikilinganishwa na Qur'an. Wanafunzi weledi katika dhana ya Hadithi na umuhimu wake, walijibu vema swali hili kwa kuchagua herufi D *Ujumbe wa hadithi ndio unaofafanua Qur'an* kwani hiyo ndio kazi kuu ya Hadithi.

Walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki baadhi yao walichagua kipotoshi A *Hadithi zilishuka mwanzo kabla ya Qur'an.* Wanafunzi hao hawakufahamu kuwa Hadithi hazikuwa zimeshuka kama Qur'an bali ni simulizi zilizotoka kwa watu ndio maana zinahakikiwa. Baadhi yao walichagua kipotoshi B *Hadithi za Mtume (s.a.w) zimeandikwa sana kuliko Qur'an.* Hoja hii si sahihi kwa sababu haina vipimo mahususi vinavyothibitisha jambo hilo. Wengine walichagua herufi C *Ujumbe wa Qur'an ndio unaofafanua Hadithi.* Kwa ujumla, waliochagua kipotoshi hiki hawakuwa na maarifa kuhusu dhana ya Hadithi wala Qur'an kwani Hadithi ni zao la utekelezaji wa Qur'an uliofanywa na Mtume (SAW) na Maswahaba wake.

Kipengele cha (ix) mwanafunzi alitakiwa kubaini aina ya Hadithi inayopatikana ikiwa Isnad imekatika. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima wanafunzi umahiri wa kuchambua aina mbalimbali za Hadithi kulingana na uchunguzi wa kisayansi. Aidha, wanafunzi mahiri katika sayansi ya Hadithi waliweza kujibu kwa usahihi na kuchagua herufi D *Ahad* kwani Hadithi hii ndio mahususi yenye sifa iliyotajwa kwenye swali. Wanafunzi walioshindwa kujibu kipengele hiki walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sayansi ya Hadithi.

Miongoni mwa wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki wapo waliochagua kipotoshi A *Maudhuu*, ambayo ni Hadithi ya uongo aliyozuliwa Mtume (SAW) na watu kwa sababu mbalimbali. Chaguo hili halikuwa sahihi kwa kuwa Hadithi maudhuu inaweza kuwa na Isnad kamili tokea asili yake (watu waliobuni) hadi wale waliopokea na kuisambaza. Wengine walichagua kipotoshi C *Dhaifu*, ambayo ni kategoria ya Hadithi inayopatikana kuwa na kasoro katika wasimulizi wake au matin yake. Wengine walichagua kipotoshi B *Hassan*, ambayo ni kategoria ya Hadithi inayokaribiana na sahihi lakini wasimulizi wake wamekuwa na udhaifu katika kumbukumbu zao.

Kipengele cha (x), mwanafunzi alitakiwa kubaini istilahi inayotumika kuonesha aina ya Hadithi iliyojengwa na maneno ya Mtume (SAW) mwenyewe kutokana na Ilham. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima wanafunzi umahiri wa kuelewa aina mbalimbali za Hadithi kulingana na sifa zake. Wanafunzi mahiri katika uchambuzi wa Hadith za Mtume (SAW) waliweza kujibu kwa usahihi kwa kuchagua herufi C *An Nabawiyyi*, kwani sifa zilizoelezwa kwenye kiulizi katika kipengele hiki zilitosheleza wasifu wa aina hiyo ya Hadithi. Aidha, wanafunzi ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika uchambuzi wa Hadithi walishindwa kubaini aina hiyo ya Hadithi iliyokusudiwa.

Miongoni mwa walioshindwa kujibu kwa usahihi kuna waliochagua kipotoshi D *Qudusiyyi* aina ambayo ni kinyume na jibu sahihi kwani *Hadithi Qudsiyy* ni ile iliyotolewa na Mtume (SAW) akimnukuu Mwenyezi-Mungu (SW) katika maneno yote bila kuongeza ya kwake. Aidha, kuna waliochagua kipotoshi B *Mutawattir* ambayo ni Hadithi yenye wapokezi wengi ambao haiwezekani kuwa wamekubaliana kusema uongo, aina hii ya Hadithi inapatikana katika kategoria ya umaarufu. Wanafunzi wengine walichagua kipotoshi A *Ash Sharif* ambayo ni hadhi ya utukufu ambayo kimsingi hadhi hiyo inaenea aina zote za Hadithi sahihi ikiwa ni Qudsiyy au Nabawiy.

Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote kumi na Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi vipengele vyote kumi.

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kisanduku.

(i) Nini kifanyike kuwasaidia Waislamu kuweza kutofautisha Hadithi sahihi na Hadithi za uongo?
- A Kuwahimiza Waislamu kuhifadhi Hadithi za Mtume (s.a.w).
- B Kusisitiza ufundishwaji wa somo la sayansi ya Hadithi.
- C Kuzingatia wanazuoni na vitendo vya Maswahaba (r.a).
- D Kuwahimiza kusoma historia ya kuzuka Hadithi za uongo.

B

(ii) Sentensi ipi kati ya zifuatazo inaonesha tofauti kati ya Sunnah na Hadithi?
- A Sunnah zipo chache na Hadithi ni nyingi.
- B Hadithi ni vitendo na Sunnah ni nadharia.
- C Sunnah ni vitendo na Hadithi ni nadharia.
- D Hadithi ni lazima kuifuata Sunnah ni hiyari.

C

(iii) Jambo gani kati ya haya linamaanisha Sunnah kivitendo?
- A Kuonja chakula kidogo.
- B Kuwapenda jamaa zako.
- C Kuuza dawa za kiarabu.
- D Kuvaa kanzu siku zote.

B

(iv) Kuna aina ngapi za Hadithi kutokana na kigezo cha umaarufu?
- A Mbili
- B Nne
- C Tatu
- D Tano

A

(v) Ni sifa gani inamtambulisha mtu mwenye nguvu kwa mujibu wa Hadithi ya Mtume (s.a.w)?
- A Mwenye kudumu na ibada ya funga.
- B Mwenye uwezo wa kupigana Jihadi.
- C Mwenye kuvumilia wakati wa shida.
- D Mwenye subira wakati wa hasira.

D

(vi) Kazi kubwa ya uandishi wa Hadithi iliyoonekana katika kipindi cha Maswahaba ni
- A Al Qatadaya
- B Al Muwatta
- C Sahihi Bukhari
- D Sahihi Muslim

A

(vii) Miongoni mwa kesi zilizoonesha umuhimu wa kuhifadhiwa Hadithi mapema baada ya kufariki Mtume (s.a.w) ni pamoja na:
- A Kuibuka kwa Mitume wa uongo.
- B Sehemu ya kuzikwa Mtume (s.a.w).
- C Usimamizi wa familia ya Mtume (s.a.w).
- D Kuhamishwa kwa makao makuu ya Kiislamu.

B

(viii) Ipi kati ya hizi zifuatazo ni sifa kubwa ya Hadithi inayoitofautisha na Qur'an?
- A Hadithi zilishuka mwanzo kabla ya Qur'an.
- B Hadithi za Mtume zimeandikwa sana kuliko Qur'an.
- C Ujumbe wa Qur'an ndio unaofafanua Hadithi.
- D Ujumbe wa Hadithi ndio unaofafanua Qur'an.

D

(ix) Ikitokea isnad imekatika inasababisha kutokea aina gani ya Hadithi?
- A Maudhuu
- B Hassan
- C Dhaifu
- D Ahad

D

(x) Ni istilahi gani hutumika kubaini aina ya Hadithi iliyojengwa na maneno ya Mtume (s.a.w) mwenyewe kutokana na ilham?
- A Ash Sharif
- B Mutawatir
- C An Nabawiyyi
- D Qudusiyyi

C

Kielelezo Na. 1.1. Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 1

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kisanduku.

(i) Nini kifanyike kuwasaidia Waislamu kuweza kutofautisha Hadithi sahihi na Hadithi za uongo?

A Kuwahimiza Waislamu kuhifadhi Hadithi za Mtume (s.a.w).
B Kusisitiza ufundishwaji wa somo la sayansi ya Hadithi.
C Kuzingatia wanazuoni na vitendo vya Maswahaba (r.a).
D Kuwahimiza kusoma historia ya kuzuka Hadithi za uongo.

[ C ]

(ii) Sentensi ipi kati ya zifuatazo inaonesha tofauti kati ya Sunnah na Hadithi?

A Sunnah zipo chache na Hadithi ni nyingi.
B Hadithi ni vitendo na Sunnah ni nadharia.
C Sunnah ni vitendo na Hadithi ni nadharia.
D Hadithi ni lazima kuifuata Sunnah ni hiyari.

[ A ]

(iii) Jambo gani kati ya haya linamaanisha Sunnah kivitendo?

A Kuonja chakula kidogo. B Kuwapenda jamaa zako.
C Kuuza dawa za kiarabu. D Kuvaa kanzu siku zote.

[ D ]

(iv) Kuna aina ngapi za Hadithi kutokana na kigezo cha umaarufu?

A Mbili B Nne
C Tatu D Tano

[ C ]

(v) Ni sifa gani inamtambulisha mtu mwenye nguvu kwa mujibu wa Hadithi ya Mtume (s.a.w)?

A Mwenye kudumu na ibada ya funga.
B Mwenye uwezo wa kupigana Jihadi.
C Mwenye kuvumilia wakati wa shida.
D Mwenye subira wakati wa hasira.

[ A ]

(vi) Kazi kubwa ya uandishi wa Hadithi iliyoonekana katika kipindi cha Maswahaba ni

A Al Qatadaya B Al Muwatta
C Sahihi Bukhari D Sahihi Muslim

[ D ]

(vii) Miongoni mwa kesi zilizoonesha umuhimu wa kuhifadhiwa Hadithi mapema baada ya kufariki Mtume (s.a.w) ni pamoja na:

A Kuibuka kwa Mitume wa uongo.
B Sehemu ya kuzikwa Mtume (s.a.w).
C Usimamizi wa familia ya Mtume (s.a.w).
D Kuhamishwa kwa makao makuu ya Kiislamu.

[ D ]

(viii) Ipi kati ya hizi zifuatazo ni sifa kubwa ya Hadithi inayoitofautisha na Qur'an?

A Hadithi zilishuka mwanzo kabla ya Qur'an.
B Hadithi za Mtume zimeandikwa sana kuliko Qur'an.
C Ujumbe wa Qur'an ndio unaofafanua Hadithi.
D Ujumbe wa Hadithi ndio unaofafanua Qur'an.

[ B ]

(ix) Ikitokea isnad imekatika inasababisha kutokea aina gani ya Hadithi?

A Maudhuu B Hassan
C Dhaifu D Ahad

[ C ]

(x) Ni istilahi gani hutumika kubaini aina ya Hadithi iliyojengwa na maneno ya Mtume (s.a.w) mwenyewe kutokana na ilham?

A Ash Sharif B Mutawatir
C An Nabawiyyi D Qudusiyyi

[ D ]


Kielelezo Na. 1.2. Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 1

### 2.1.2 Swali la 2: Tawhiid

Swali hili lilitoka katika mada za Tawhiid ambazo ni *Dhana ya elimu katika uislamu, Mgawanyo wa Elimu (Elimu ya Mazingira na Muongozo), Nguzo za Imani ya kiislamu, Dhana ya dini kwa mujibu wa Qur'an na Njia za kumjua Mwenyezi Mungu (s.w).* Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kuoanisha maelezo katika orodha A (i) - (x) na maneno stahiki kutoka orodha B (A - O), kisha kujaza herufi ya jibu sahihi katika jedwali alilopewa. Swali lilipima umahir wa wanafunzi katika kuelewa dhana mabalimbali muhimu za kiitikadi ambazo anapaswa kuzizingatia katika maisha yake ya kila siku. Kila kipengele katika swali kilikuwa na alama (01) hivyo swali lote lilikuwa na jumla ya alama 10. Vipengele vya kuonisha vilikuwa kama ifuatavyo:

| Orodha A | | Orodha B | |
|---|---|---|---|
| (i) | Hisia za kimaumbile zinazomuongoza mja kutambua uwepo wa Mwenyezi Mungu. | A | Muislamu |
| | | B | Kuamini ghaibu. |
| (ii) | Viumbe wa kiroho wasio na miili wala matashi ya kimaumbile. | C | Ri'a |
| (iii) | Kurasa zenye maandishi alizopewa Nabii Ibrahim (a.s) kuongoza watu wake. | D | Utawa |
| (iv) | Elimu ya ujenzi inayomuwezesha mtu kusanifu na kusimamia majengo ya makazi na ibada. | E | Wahyi |
| | | F | Ushirikina |
| (v) | Watu miongoni mwa wanaume walioteuliwa na Mwenyezi Mungu (s.w) ili wafikishe ujumbe wake kwa wengine. | G | Allah (s.w) |
| | | H | Washirikina |
| (vi) | Ujumbe wa Mwenyezi Mungu uliotufikia kwa njia ya il-hamu, nyuma ya pazia, Malaika, ndoto za kweli na maandiko. | I | Faradh Ain |
| | | J | Mitume |
| (vii) | Utaratibu wa maisha ambao wafuasi wake wanajitenga na harakati za kumletea mwanadamu maendeleo ya hapa duniani. | K | Fitrah |
| | | L | Elimu |
| (viii) | Kukubali kuwepo Allah (s.w), Malaika wake, siku ya kiama pamoja na Pepo na Moto. | M | Faradh kifaya |
| (ix) | Ibada unayofanya ili watu katika jamii wajue na kukuona. | N | Suhufi |
| | | O | Malaika |
| (x) | Kumpa kiumbe sifa anayostahiki Mwenyezi Mungu (s.w) pekee. | | |

Swali lilijibiwa na wanafunzi wote 85,565 (100%) waliofanya upimaji huu, ambapo kati yao wanafunzi 50,826 (59.40%) walipata alama 3 hadi 6 ambazo ni alama za wastani. Wanafunzi 19,587 (22.89%) walipata alama 7 hadi 10 ambazo ni alama za juu za ufaulu. Aidha, wanafunzi 15152 (17.71%) walipata alama za chini kuanzia 0 hadi 2. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao umeoneshwa katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2**. *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 2*

Chati Na. 2 inaonesha ufaulu mzuri katika swali hili kwa kuwa kati ya wanafunzi wote waliofanya upimaji huu asilimia 82.29 waliweza kujibu kwa usahihi dhidi ya asilimia 17.71 walioshindwa.

Aidha, ufaulu huo mzuri katika swali hili ulichangiwa na wanafunzi wengi kuwa maarifa ya kutosha katika dhana mbalimbali za itikadi ya Uislamu (Tawhiid) kama ilivyobainishwa katika uchambuzi wa majibu ya wanafunzi hao katika kila kipengele:

Kipengele cha (i) mwanafunzi alitakiwa kubaini hisia za kimaumbile zinazomwongoza mja kutambua uwepo wa Mwenyezi Mungu. Wanafunzi mahiri katika njia za kumjua Mwenyezi-Mungu walielewa vema matakwa ya kipengele hiki na kuoanisha kwa usahihi na herufi K *Fitrah.* Wanafunzi hao walielewa maelezo yaliyotolewa katika kipengele hiki na kuweza kujibu kwa usahihi. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki baadhi yao walichagua herufi E *Wahyi* ambao ni ufunuo wa hakika na wengine walichagua herufi L *Elimu*, Wanafunzi hao

walishindwa kuelewa matakwa ya kipengele hiki kwa kuwa machaguo yote hayo sio *Hisia* kama ilivyoelezewa katika hoja ya kipengele hiki.

Kipengele cha (ii), mwanafunzi alitakiwa kubaini viumbe wa kiroho wasio na mwili wala matashi ya kimaumbile.Wanafunzi weledi katika nguzo za Imani ya kiislamu waliweza kujibu kwa usahihi katika kipengele kwa kuchagua herufi O *Malaika*. Wanafunzi hawa walielewa vema sifa za Malaika hivyo waliweza kuonisha kwa usahihi. Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki, miongoni mwao walichagua herufi N S*uhufi* ambazo ni kurasa zenye maandishi ya ya muongozo walizopewa Manabii na wengine walichagua herufi H *Washirikina*, ambalo ni kundi la watu (wafuasi) wanaoamini kuwepo kwa miungu wengi. Kwa ujumla wanafunzi walioshindwa kujibu kipengele hiki walionesha kutokuwa na maarifa ya nguzo za Imani ya kiislamu, hususani nguzo ya pili.

Kipengele cha (iii), mwanafunzi alitakiwa kubaini kurasa zenye maandishi alizopewa nabii Ibrahim (AS) kuongoza watu wake. Wanafunzi walioelewa vizuri mada ya nguzo za Imani ya kiislamu waliweza kujibu kwa usahihi na kuchagua herufi N *Suhufi*, ambazo kihistoria walipewa manabii wawili ambao ni Ibrahim na Musa (AS). Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki baadhi walichagua kipotoshi C *Ria*, ambayo ni kufanya jambo ili watu wakusifie au wakuone. Wanafunzi hawa walionesha kutokuwa na maarifa katika nguzo ya tatu ya imani ya Kiislamu hivyo walishindwa kujibu kwa usahihi.

Kipengele cha (iv), mwanafunzi alitakiwa kubaini hukumu ya elimu ya ujenzi inayomuwezesha mtu kusanifu na kusimamia majengo ya makazi na ibada. Wanafunzi mahiri katika dhana ya elimu katika Uislamu waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki kwa kuchagua herufi M *Faradh kifaya,* kwa kuwa elimu hiyo ni lazima kwa baadhi ya watu kuwa nayo katika jamii ili kufanikisha mahitaji yao. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki, baadhi yao walichagua herufi C *Ria*, (kujionesha ukiwa unafanya jambo) na wengine walichagua herufi N *Suhufi*, kurasa za mwongozo walizopewa manabii wawili. Hali hii inadhihirisha kwamba hawakuwa na maarifa kuhusu dhana ya mgawanyo wa Elimu katika faradhi kifaya na Faradh ain.

Kipengele cha (v), mwanafunzi alitakiwa kubaini cheo au nafasi ya watu miongoni mwa wanaume walioteuliwa na Mwenyezi Mungu (s.w) ili wafikishe ujumbe wake kwa wengine. Wanafunzi walioelewa vema nguzo ya nne ya imani ya Kiislamu (kuamini Mitume) waliweza kujibu vema kwa kuchagua herufi J *Mitume* kwa kuwa maelezo yaliyotolewa katika kipengele cha (v) yalitoa taarifu ya Mitume wa Mwenyezi-Mungu. Ama wanafunzi waliokosa katika kipengele hiki baadhi yao walichagua herufi A *Muislamu,* jambo lililoonesha kuwa walishindwa kuelewa hoja ya kipengele hiki kwani Muislamu ni cheo au hadhi inayoenea watu wa jinsia zote. Wengine walichagua herufi N *Suhufi* (kurasa za muongozo walizopewa manabii wawili) na K *Fitra*. (hisia zinazomuongoza mja kumjua Mungu). Wanafunzi hawa walionesha kutokuwa na maarifa kuhusu nguzo ya nne ya Imani ya Kiislamu inayofundisha kuamini Mitume wa Mwenyezi-Mungu.

Kipengele cha (vi), mwanafunzi alitakiwa kubaini jina mahususi linalotambulisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu uliotufikia kwa njia ya Ilhamu, nyuma ya pazia, malaika, ndoto za kweli na maandiko. Wanafunzi mahiri juu ya dhana ya elimu katika Uislamu waliweza kujibu kipengele hiki kwa usahihi kwa kuchagua herufi E *Wahyi* kwani njia zilizotajwa katika maelezo ya kipengele hiki zilibainisha namna ufunuo ulivyoweza kuwafikia wanadamu. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kipengele hiki baadhi walichagua herufi K *Fitrah* (hisia za kumjua Mwenyezi-Mungu). Hao walishindwa kuelewa kwamba Fitrah zinaweza kuwa katika njia mbili kubwa katika njia zilizotajwa nazo ni ilham na ndoto za kweli hivo haitoshi kuwa jibu sahihi. Wengine walichagua herufi L *Elimu*, ambalo ni jina la jumla linaloenea maarifa yote ya mazingira na mwongozo ambayo pamoja na kuwa na asili au chanzo kimoja katika njia hizo yenyewe ni zao la Wahyi.

Kipengele cha (vii), mwanafunzi alitakiwa kubaini jina la utaratibu wa maisha ambao wafuasi wake wanajitenga na harakati za kumletea mwanadamu maendeleo ya hapa duniani. Jibu sahihi la kipengele hiki lilikuwa D *Utawa*, ambapo wanafunzi waliokuwa na maarifa juu ya dhana ya Dini za watu waliweza kuoanisha kwa usahihi. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kipengele hiki baadhi yao walichagua herufi F *Ushirikina* jambo lililoonesha kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sifa za Dini za watu kwani Ushirikiana ni aina ya Dini ambayo

wafuasi wake wanaamini kuwepo kwa miungu wengi. Wanafunzi wengine walichagua herufi H *Washirikina*, ambao ni jina la wafuasi wa Dini ya Ushirikina na sio jina la Dini kama hoja ya kipengele hiki ilivyotaka.

Kipengele cha (viii), mwanafunzi alitakiwa kubaini dhana jumuishi katika kukubali kuwepo kwa Allah (s.w), Malaika wake, siku ya kiama, pamoja na pepo na moto. Wanafunzi mahiri katika nguzo za Imani ya Kiislamu waliweza kujibu kwa usahihi kwa kuchagua herufi B *Kuamini ghaibu* kwa kuwa yote yaliyotajwa katika maelezo hayo ni yale yasiyoonekana kwa macho bali yanathibitika kwa mantiki. Wanafunzi ambao walishindwa kujibu kipengele hiki walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika itikadi ya Uislamu ambayo ni msingi mkubwa wa Dini. Baadhi yao walichagua herufi K *Fitrah*. (hisia za kutambua kuwepo kwa Mungu). Wanafunzi hao walishindwa kujua kuwa hisia hizo hazitambui uwepo wa Malaika wala moto na Pepo. Wengine walichagua herufi F *Ushirikina* dhana ambayo ilikuwa kinyume na itikadi iliyoelezwa katika kipengele hiki.

Kipengele cha (ix), mwanafunzi alitakiwa kubaini dhana inayopatikana katika ibada inayofanywa ili watu katika jamii wajue na kukuona. Wanafunzi walioelewa vema dhana ya Shahada waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki na kuchagua herufi C *Ria*. Wanafunzi hawa walielewa vizuri kuwa ibada zote zinapaswa kufanywa kwa kutarajia malipo kwa Allah (SW) pekee na si vinginevyo. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kipengele hiki walichagua herufi I *Faradh Ain*, jawabu ambalo ni tofauti na maelezo ya kipengele hiki kwani Faradh Ain ni jambo au ibada ya lazima kutekelezwa na kila mtu binafsi.

Kipengele cha (x), mwanafunzi alitakiwa kubaini dhana ya kumpa kiumbe sifa anayostahiki Mwenyezi Mungu (SW) pekee. Wanafunzi walio elewa vema itikadi ya Uislamu waliweza kujibu kipengele hiki kwa usahihi kwa kuchagua herufi F *Ushirikina* kwa kuwa kitendo hicho ni kinyume na itikadi ya Tawhiid hivyo mtu yoyote akifanya anaingia katika Dini ya ushirikina. Ama wanafunzi walioshindwa kujibu kipengele hiki, wengi walichagua herufi N *Suhufi* wanafunzi hawa walionesha kutokuwa na maarifa kuhusu itikadi ya Uislamu kwa ujumla kwani maelezo ya kipengele hiki yametoka katika nguzo ya kwanza ya Imani wakati Suhufi ni habari

inayotoka katika nguzo ya tatu ya Uislamu. Suhufi ni kurasa za mwongozo walizopewa nabii Ibrahim na Musa.

Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi katika vipengele vyote kumi na Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika vipengele vyote kumi.

| Orodha A | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Orodha B | K | O | N | M | J | E | D | B | C | F |

Kielelezo Na. 2.1. Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 2

| Orodha A | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Orodha B | C | A | B | D | O | K | M | I | H | G |

Kielelezo Na. 2.2. Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 2

## 2.2 Sehemu B: Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3, 4 na 5) yenye jumla ya alama arobaini (40) na mwanafunzi alipaswa kujibu maswali yote.

### 2.2.1 Swali la 3: Tawhiid

Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kuandika **Kweli** kama sentensi ni sahihi au **Si kweli** ikiwa sentensi siyo sahihi katika vipengele (i hadi x). Kila kipengele kilikuwa na alama moja (01) hivyo swali lote lilikuwa na jumla ya alama kumi (10). Swali hili lilipima umahiri wa wanafunzi kuelewa dhana mbalimbali za itikadi ya Uislamu kama zinavyoonekana katika vipengele vifuatavyo:

3. Andika **KWELI** kama sentensi ni sahihi au **SI KWELI** ikiwa sentensi si sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Kuamini Malaika kuna athari katika tabia na mwenendo wa mja ……………………….

(ii) Idadi ya vitabu vyote alivyovishusha Mwenyezi Mungu (s.w) haijulikani ……………

(iii) Miongoni mwa sifa za Mitume ni kuwa na elimu ya hali ya juu kuliko watu wote wa enzi zao…………………………

(iv) Kuamini siku ya mwisho ni tofauti na kuamini maisha baada ya kufa …………………

(v) Anaeamini Qadar hapaswi kujishughulisha sana kwa kuwa anajua kila kitu kimepangwa ………………………………….

(vi) Uislamu unakubali kuwa jamii nyingi za kiafrika zina watu wenye dini na watu wasiokuwa na dini …………………………………


(vii) Itiqadi, uchumi, utamaduni na hata siasa yote hayo ni katika dini ……………………

(viii) Hapa duniani kuna dini mbili tu, ya Ukristo na Uislamu…………………………………..

(ix) Kila mtu duniani ana Mungu anayemuamini na kumfuata ………………………………

(x) Kuna maisha ya Bar-zakh na Maisha ya Kaburini baada ya mwanadamu kufariki ………………………………………

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi wote 85,565 (100%) waliosajiliwa katika upimaji huu ambapo kati yao, wanafunzi 71,406 (83.45%) walipata alama 3 hadi 6 ambazo ni alama za wastani. Wanafunzi 7,158 (8.37%) walipata alama za chini kuanzia 0 hadi 2 na wanafunzi 7,001 (8.18%) walipata alama 7 hadi 10 ambazo ni alama za juu za ufaulu. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao umeoneshwa katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3**. *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha ufaulu mzuri katika swali hili kwa kuwa kati ya wanafunzi wote waliofanya upimaji huu asilimia 91.63 waliweza kujibu kwa usahihi dhidi ya asilimia 8.37 walioshindwa.

Aidha, ufaulu huo mzuri katika swali hili ulichangiwa na wanafunzi wengi kuwa maarifa ya kutosha katika dhana mbalimbali za itikadi ya Uislamu (Tawhiid) kama ilivyobainishwa katika uchambuzi wa majibu ya wanafunzi hao katika kila kipengele:

Katika kipengele cha (i), mwanafunzi alitakiwa kujibu hoja kuwa, imani juu ya malaika ina athari katika tabia na mwenendo wa mja. Wanafunzi mahiri katika dhana ya kuamini Malaika waliweza kujibu kwa usahihi hoja hiyo kwa kuthibitisha kuwa ni Kweli, kwani imani hiyo inabadilisha mtindo wa maisha wa mtu yeyote anayeikubali. Aidha, wanafunzi waliokanusha hoja hiyo walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya itikadi ya Uislamu juu ya Malaika.

Kipengele cha (ii), kilikuwa na hoja kuwa, idadi ya vitabu vyote alivyovishusha Mwenyezi Mungu haijulikani. Katika hoja hiyo wanafunzi walioelewa vema itikadi kuhusu Mitume na historia yao walijibu kwa usahihi kwa kukubali kuwa ni Kweli. Ni hakika kuwa hakuna anayejua

idadi kamili ya vitabu vya Mwenyezi-Mungu kwa kuwa haijatajwa kwenye Qur'an. Aidha, waliopinga hoja hiyo hawakuweza kutofautisha baina ya vitabu mahususi vilivyotajwa kwenye Qur'an na dhana ya idadi kamili ya vitabu vya Mwenyezi-Mungu (SW) kama ilivyoelezwa kwenye hoja ya kipengele hiki.

Kipengele cha (iii), kilikuwa na hoja kuwa, miongoni mwa sifa za Mitume ni kuwa na elimu ya hali ya juu kuliko watu wote wa enzi zao. Jibu sahihi la hoja hii lilikuwa ni Kweli. Wanafunzi mahiri katika nguzo ya kuamini Mitume waliweza kujibu kwa usahihi kwa kuthibitisha kuwa ni Kweli. Wanafunzi hao walielewa kuwa Mitume walipewa nafasi ya kuwasilina na Mwenyezi-Mungu bila kizuizi hivyo wasingeweza kufanana na yeyote yule katika wafuasi wao kielimu. Aidha, waliokanusha hoja hii walishindwa kuelewa vizuri habari ya Nabii Musa na Khidhr ambaye alionekana kuwa na elimu ya ziada (ghaibu) kuliko Musa, kwani Musa yeye alipewa kaumu kuiongoza tofauti na Khidhr (AS) hivyo alikuwa na ziada ya mwongozo (kitabu na sheria).

Kipengele cha (iv), kilikuwa na hoja kuwa, "Kuamini siku ya mwisho ni tofauti na kuamini maisha ya baada ya kufa". Hoja hii ilikusudiwa kupima uwezo wa mwanafunzi kuelewa nguzo ya tano ya imani ya Kiislamu, ambapo wanafunzi mahiri katika mada ya Nguzo za Imani ya Kiislamu walipinga hoja hiyo kwa kuandika kuwa Si kweli. Wanafunzi hao walielewa kuwa yote hayo yanakutana katika msingi wa kukubali Akhera hivyo hakuna tofauti yoyote. Aidha, wanafunzi waliokubali hoja hiyo walichanganya dhana ya maisha baada ya kufa na Barzakh (maisha ya kaburini) bila ya kuzingatia kuwa hiyo ni hatua mojawapo katika hatua za maisha baada ya kufa. Maisha baada ya kufa yanagusa sehemu au hatua nne ambazo ni Barzakh, Kufufuliwa, Kuhukumiwa na mwishowe kuishi peponi au motoni.

Kipengele cha (v), kilikuwa na hoja kuwa, anayeamini Qadar hapaswi kujishughulisha sana kwa kuwa anajua kila kitu kimepangwa. Wanafunzi walioelewa vema dhana ya Qadar walipinga hoja hii kwa kujibu kuwa Si Kweli, kwani Qadar ya Mwenyezi-Mungu hakuna anayeijua bali watu wote wamepewa kanuni za wazi za kimaumbile ambazo wanahiyari ya kuzifuata ikiwa wanamahitaji yao hivyo kama mtu akizifuata atapata matokeo na akiziacha hatopata mafanikio. Hoja hii ilijengwa katika msingi wa

kueleweka vibaya kwa dhana ya Qadar. Aidha, wanafunzi waliokubali hoja hiyo walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nguzo ya Qadar hivyo walishindwa kubaini kuwa huo ni mtazamo potofu juu ya dhana hii.

Kipengele cha (vi) kilikuwa na hoja kuwa, Uislamu unakubali kuwa jamii nyingi za kiafrika zina watu wenye dini na wasiokuwa na dini. Wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu walikanusha hoja hii na kujibu kuwa Si Kweli. Wanafunzi hao walielewa kuwa, hakuna mtu au jamii ambayo haina Dini kwani kwa mujibu wa Uislamu Dini ni mfumo wa maisha hivyo hakuna jamii ambayo haina utaratibu wa maisha. Aidha, wanafunzi waliokubali hoja hii walionesha kutokuwa na maarifa juu ya dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu na kujibu hoja hii kutokana na uzoefu wao.

Kipengele cha (vii) kilikuwa na hoja kuwa; Itikadi, uchumi, utamaduni na hata siasa yote ni katika dini. Wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu walikubali hoja hii na kujibu kuwa ni Kweli. Wanafunzi hao walielewa kuwa Dini ni mfumo au utaratibu wa maisha ya watu hivyo dhana ya Itikadi, uchumi, utamaduni na hata siasa ni sehemu katika mifumo wanayoishi hivyo haviwezi kutenganishwa na Dini. Kwa upande mwingine wanafunzi ambao hawakuwa na maarifa juu ya dhana ya Dini walipinga hoja hiyo kutokana na kupishana na kile wanachodhani kuwa ndio Dini pekee kama vile Kusali, Kufunga Ramadhani na Kuhiji. Jambo ambalo wengi hawafahamu ni kwamba ibada maalumu ni sehemu tu katika Dini na sio ukamilifu wa Dini yenyewe.

Kipengele cha (viii) kilikuwa na hoja kuwa, hapa duniani kuna dini mbili tu, Ukristo na Uislamu. Wanafunzi mahiri katika dhana ya Dini hawakukubali hoja hiyo kwa kuandika kuwa Si Kweli. Wanafunzi hao walielewa vema kuwa Dini kama utaratibu wa maisha ya watu hapa duniani haiwezi kuwa mbili tu kwani wapo watu ambao hawakubaliani na Ukristo wala Uislamu na kujichagulia utaratibu wao mwengine k.v Budha, Wahindu na Majusi. Aidha, wanafunzi waliokubali hoja hii walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya Dini na kuwa wameathirika na mazingira wakiwaona wafuasi wengi wa Dini katika jamii zao ni ama Waislamu au Wakristo.

Kipengele cha (ix) kilikuwa na hoja kuwa, kila mtu duniani ana Mungu anayemuamini na kumfuata. Katika hoja hii wanafunzi mahiri katika dhana ya Dini walithibitisha kuwa ni Kweli, kwani kwa mujibu wa Uislamu dhana ya mungu inatafsiriwa kuwa yeyote au chochote kinachoabudiwa na kufuatwa (kutiiwa) na mwanadamu katika maisha yake kama ilivyobainishwa katika Qur'an (25:43) au (9:31). Katika Qur'an (25:43) Mwenyezi-Mungu anaeleza kuwa; "*Je, umemuona yule anayefanya matamanio yake (kile anachokipenda) kuwa Mungu wake…"* Aya hii inathibitisha kuwa ni sahihi kwamba kila mtu anaye Mungu anayemuamini na kumfuata, tofauti ni kwamba wapo wanaoamini Mungu muumba na wengine wanaamini Miungu iliyoumbwa. Aidha, wanafunzi waliokanusha hoja hii walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu hivyo walishindwa kubaini ukweli huo.

Kipengele cha (x) kilikuwa na hoja kuwa, kuna maisha ya barzakh na maisha ya kaburini baada ya mwanadamu kufariki. Wanafunzi walioelewa vema nguzo ya tano ya imani ya Kiislamu walikanusha hoja hiyo na kujibu kuwa Si kweli. Wanafunzi hao walielewa dhana ya Barzakh kuwa ni maisha ya kaburini ambayo ni hatua ya pili ya kuelekea maisha ya akhera, hivyo Barzakh na maisha ya kaburini ni kitu kimoja (hakuna tofauti). Aidha, wanafunzi waliokubali hoja hiyo walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nguzo ya tano ya imani ya Kiislamu hivyo walijibu hoja hiyo kwa kutofautisha dhana hizo kwakuwa hawakujua maana ya Barzakh.

### 2.2.2 Swali la 4: Tarekh

Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kujaza nafasi zilizo wazi katika kila kipengele (a) – (j) kwa kutumia maneno sahihi aliyopewa kwenye kisanduku. Swali lilipima umahiri wa wanafunzi kukumbuka matukio na sehemu muhimu katika Historia ya Uislamu hasa katika kipindi cha Makka. Kila kipengele kilikuwa na uzito wa alama 2 hivyo, jumla ya alama zote katika swali zilikuwa 20. Swali hilo lilikuwa kama ifuatavyo;

4. Kwa kutumia maneno uliyopewa katika kisanduku, chagua jibu sahihi ili kujaza nafasi zilizo wazi katika vipengele (a) – (j).

| |
|---|
| Ushirikina, Makkah, Zam-zam, Al-Ka'abah, Hijaz, Baytul Atiq, Jahiliyyah, Madinah, Ismail (a.s), Ukristo, Jeddah, Ummul-Qura, Baytul Maqdis, Abu Talib, Jabal Hira. |

(a) Zama ambazo watu wa arabuni na sehemu zingine walikuwa wakiishi kwa kufuata matashi yao kinyume na mwongozo wa Allah (s.w) ni..........................................

(b) Kabla ya kuitwa Saud Arabia nchi aliyozaliwa Mtume (s.a.w) ilikuwa inajulikana kwa jina la..............................................

(c) Mji ulioanzishwa na Nabii Ibrahim (a.s) na familia yake kwa amri ya Allah (s.w) unajulikana kwa jina la ......................................

(d) Kabla ya kuja Uislamu Waarabu na watu wa sehemu zingine duniani walizama katika dini ya ..............................................

(e) Kutokana na ukongwe wa nyumba ya kwanza ya ibada iliyojengwa na nabii Ibrahiim (a.s) nyumba hiyo imeitwa kwa jina la ......................................

(f) Mwanzo wa kukua kwa mji wa Bakkah kwa kiasi kikubwa kulichangiwa na kuwepo kwa ....................................


(g) Mji wa Makkah umekuwa mtukufu kwa sababu ya ....................................

(h) Kutokana na utukufu wake Mji wa Makkah umeitwa katika Qur'an kwa jina la ...................................

(i) Uelekeo (kibla) wa kwanza wa ibada za Waislamu ulikuwa ...............................

(j) Kiongozi wa kwanza wa mji wa Makkah ambae ni katika mababu wa Mtume (s.a.w) ni ......................................

Swali lilijibiwa na wanafunzi wote 85,565 (100%) waliofanya upimaji, ambapo kati yao wanafunzi 62,118 (72.60%) walipata alama 0 hadi 4 ambao ni ufaulu hafifu. Wanafunzi 22,492 (26.29%) walipata alama za wastani kuanzia 5 hadi 12 na wanafunzi 955 (1.12%) walipata alama 13 hadi 20 ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao umeoneshwa katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4**. *Asilimia ya Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4.*

Chati Na. 4 inaonesha ufaulu hafifu katika swali hili kwa kuwa kati ya wanafunzi wote waliofanya upimaji huu ni asilimia 27.40 pekee ndio waliweza kujibu kwa usahihi dhidi ya asilimia 72.59 walioshindwa.

Aidha, ufaulu huo hafifu katika swali hili ulichangiwa na wanafunzi wengi kukosa maarifa ya kutosha katika mada ya Bara Arab zama za Jahiliyyah kama ilivyooneshwa katika uchambuzi wa majibu ya wanafunzi hao katika kila kipengele:

Katika kipengele (a) mwanafunzi alitakiwa kubaini jina la zama ambazo watu walikuwa wakiishi kwa kufuata matashi yao kinyume na mwongozo wa Allah (s.w). Wanafunzi mahiri katika historia kabla ya Mtume (SAW) waliweza kujibu kuwa ni *Jahiliyyah*, hiki ni kipindi ambacho mafundisho ya Mwenyezi-Mungu yalipotea na ulimwengu kuwa katika giza. Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki baadhi yao waliandika *Ukristo* na wengine *Ushirikina* ambazo ni majina ya Dini. Wanafunzi hao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu historia kabla ya kuja Mtume (SAW) hivyo walichanganya maelezo ya kipengele hicho na aina za Dini.

Kipengele (b) mwanafunzi alitakiwa kutaja jina la nchi aliyozaliwa Mtume (SAW) kabla ya kuitwa Saud Arabia. Wanafunzi mahiri katika historia kabla ya utume wa Muhammad (SAW) waliweza kujbu kwa usahihi kuwa ni *Hijaz.* Kwa upande wa wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi baadhi walichagua jina la *Makkah.* Wanafunzi hao walishindwa kuelewa kuwa Makkah ni jina la mji na sio nchi.

Kipengele (c) mwanafunzi alitakiwa kubainisha jina la mji ulioanzishwa na Nabii Ibrahimu (AS) na familia yake kwa amri ya Allah (SW). Wanafunzi mahiri katika historia ya Ibrahim (AS) waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki kwa kuandika jina *Makkah* kwani historia inabainisha wazi kuwa ni yeye Ibrahim aliyehuisha tena mji wa Makkah baada ya kuiacha familia yake hapo kwa amri ya Mwenyezi-Mungu (SW) kama ilivyobainishwa katika Qur'an "*Mola wetu, hakika mimi nimeweka baadhi ya kizazi changu (Mwanangu Ismail na mama yake Hajrah) katika bonde hili la Makkah lisilokuwa na mimea yoyote kwenye nyumba yako tukufu….." (14:37)*. Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi baadhi yao waliandika *Madinah* ambao ni mji ulioanzishwa miaka mingi baadae na baadhi ya makabila ya Waarabu na Wayahudi. Wengine waliandika *Al-Qaabah* baada ya kushindwa kuelewa vema swali kwani Al-Qaabah ni nyumba ya ibada na sio jina la mji kama ilivyobainishwa katika matakwa ya kipengele hiki.

Kipengele (d) mwanafunzi alitakiwa kubaini dini ambayo waarabu na watu wa sehemu zingine walikuwa nayo kabla ya Uislamu. Wanafunzi mahiri katika historia ya Uislamu kabla ya kuja Mtume Muhammad (SAW) waliweza kujibu kwa usahihi kuwa ni *Ushirikina*. Katika zama hizo watu wengi waliabudu sanamu walizounda kwa ajili ya kuomba mambo yao mbalimbali. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kipengele hiki wengi wao walichagua neno *Ukristo* kwa dhana kuwa Nabii Muhammad (SAW) alikuja baada ya Isa (AS). Wengine walijibu kuwa ni Ummul Qura. Wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika historia kwa ujumla kwani jina Ummul Qura ni jina la mji wa Makkah lenye maana ya mama wa miji yote.

Kipengele (e) mwanafunzi alitakiwa kutaja jina la nyumba ya ibada iliyojengwa na Nabii Ibrahiim kutokana na ukongwe wake. Wanafunzi walioelewa vizuri historia ya mji wa Makkah ambayo ndani yake

imejengwa nyumba hiyo waliweza kujibu kwa usahihi kuwa ni *Baitul atiq* ambalo ni jina linalotumika kuitukuza nyumba hii tukufu (Al-Qaabah). Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki baadhi yao waliandika neno *Al kaaba* ambalo ni jina halisi la nyumba hiyo kinyume na maelezo yaliyotolewa katika kipengele hiki yaliyotoa sifa ya ukongwe.

Kipengele (f) mwanafunzi alitakiwa kutaja sababu ya kukua kwa mji wa Bakkah hapo mwanzo ambapo wanafunzi mahiri katika kuchambua historia ya Makkah waliweza kujibu kwa usahihi kuwa ni *Zamzam*. Wanafunzi hao walikumbuka vema mchango wa chemchem ya Zamzam ambayo iliwavutia wahamiaji kuja kuishi sehemu hiyo kwa idhini ya familia ya Ibrahim (AS). Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki baadhi yao waliandika *Abu Talib* na wengine *Ismail* ambao wote walikuwa viongozi wa mji wa Bakkah katika vipindi tofauti. Hata hivyo, haikuwa sababu ya uongozi wao uliosababisha kukua kwa mji wa Bakkah hususani wakati wa mwanzo wa historia yake.

Kipengele (g) mwanafunzi alitakiwa ataje sababu ya utukufu (kutukuzwa) kwa mji wa Makkah. Wanafunzi walioelewa vema historia ya mji wa Makkah waliweza kujibu kwa sahihi kuwa ni kuwepo kwa *Al kaaba*. Pamoja na matukio mengine ya kihistoria yaliyojiri katika mji wa Makkah lakini kuwepo kwa nyumba hii ya kwanza kwa wanadamu kufanya ibada (kumtukuza Allah (SW)) ndani yake ndio sababu kuu ya utukufu wake. Hata hivyo, wanafunzi ambao hawakuifahamu historia ya mji wa Makkah vizuri, walishindwa kujibu kwa usahihi. Baadhi yao walijibu kuwa ni *Hijaz* ambalo ni jina la zamani la nchi ya Saud Arabia ambalo halina uhusiano na utukufu wa mji wa Makkah. Wengine walijibu kuwa ni *Zamzam,* chemchem ya maji iliyopo katika mji wa Makkah ambayo pamoja na historia yake njema ya kuanza kwake lakini haijafikia hadhi ya *Al kaaba* tukufu.

Kipengele (h) mwanafunzi alitakiwa kutaja jina la mji wa Makkah kutokana na utukufu wake kama ulivyotajwa katika Qur’an. Wanafunzi mahiri katika historia ya mji wa Makkah waliweza kujibu kwa usahihi kuwa ni *Ummul Qura* lenye maana ya mama wa miji yote. Hii ni kutokana na historia yake kubwa (tukufu) tangu Nabii Adam (AS) hadi Muhammad (SAW). Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika

kipengele hiki baadhi yao walijibu *Baytul Maqdis* ambalo ni jina mahususi kwa msikiti uliopo Jerusalem nchini Palestina ambao unahadhi ya tatu ya utukufu duniani.

Kipengele (i) mwanafunzi alitakiwa kubainisha uelekeo wa kwanza wakati wa ibada za Waislamu. Wanafunzi mahiri wa historia waliweza kujibu kwa usahihi kipengele hiki kuwa ni *Baytul Maqdis* msikiti wa kihistoria uliojengwa tokea zama za Nabii Suleiman uliopo Jerusalem Palestina. Wanafunzi wengine walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki waliandika *Baytul Atiq.* Wanafunzi hao walionesha kuwa hawana maarifa juu ya historia kwa ujumla kwani *Baytul Atiq* ni jina miongoni mwa majina ya *Al kaabah* iliyopo Makkah ambayo ndiyo Qibla au uelekeo wa sasa wa ibada za Waislamu.

Kipengele (j) mwanafunzi alitakiwa kutaja jina la kiongozi wa kwanza wa mji wa Makkah ambaye ni katika mababu wa Mtume (SAW). Jibu sahihi katika kipengele hiki lilikuwa ni *Ismail,* ambapo wanafunzi mahiri katika historia waliweza kubaini kutokana na nasabu ya Mtume (SAW) mwenyewe na historia ya kuanzishwa na kukua kwa mji wa Makkah. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi wengine waliandika *Abu Talib,* wanafunzi hao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu historia ya Makkah kwani Abu Talib hakuwa kiongozi wa mwanzo wa Makkah pia si katika mababu wa Mtume (SAW) bali ni baba yake mdogo (mdogo wa baba yake mzazi).

Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kujibu kwa usahihi katika vipengele vyote na Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika vipengele vyote vya swali.

4. Kwa kutumia maneno uliyopewa katika kisanduku, chagua jibu sahihi ili kujaza nafasi zilizo wazi katika vipengele (a) – (j).

| |
|---|
| Ushirikina, Makkah, Zam-zam, Al-Ka'abah, Hijaz, Baytul Atiq, Jahiliyyah, Madinah, Ismail (a.s), Ukristo, Jeddah, Ummul-Qura, Baytul Maqdis, Abu Talib, Jabal Hira. |

(a) Zama ambazo watu wa arabuni na sehemu zingine walikuwa wakiishi kwa kufuata matashi yao kinyume na mwongozo wa Allah (s.w) ni....Jahiliyyah....

(b) Kabla ya kuitwa Saud Arabia nchi aliyozaliwa Mtume (s.a.w) ilikuwa inajulikana kwa jina la....Hijaz....

(c) Mji ulioanzishwa na Nabii Ibrahim (a.s) na familia yake kwa amri ya Allah (s.w) unajulikana kwa jina la ....Makkah....

(d) Kabla ya kuja Uislamu Waarabu na watu wa sehemu zingine duniani walizama katika dini ya ....Ushiríkina....

(e) Kutokana na ukongwe wa nyumba ya kwanza ya ibada iliyojengwa na nabii Ibrahiim (a.s) nyumba hiyo imeitwa kwa jina la ....Baytul Atiq....

(f) Mwanzo wa kukua kwa mji wa Bakkah kwa kiasi kikubwa kulichangiwa na kuwepo kwa ....Zam zam....

(g) Mji wa Makkah umekuwa mtukufu kwa sababu ya ....Al-Kaabah....

(h) Kutokana na utukufu wake Mji wa Makkah umeitwa katika Qur'an kwa jina la ....Ummul-Qura....

(i) Uelekeo (kibla) wa kwanza wa ibada za Waislamu ulikuwa ....Baytul maqdis....

(j) Kiongozi wa kwanza wa mji wa Makkah ambae ni katika mababu wa Mtume (s.a.w) ni ....Ismail (a.s)....

Kielelezo Na. 4.1. Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 4

4. Kwa kutumia maneno uliyopewa katika kisanduku, chagua jibu sahihi ili kujaza nafasi zilizo wazi katika vipengele (a) – (j).

| |
|---|
| Ushirikina, Makkah, Zam-zam, Al-Ka'abah, Hijaz, Baytul Atiq, Jahiliyyah, Madinah, Ismail (a.s), Ukristo, Jeddah, Ummul-Qura, Baytul Maqdis, Abu Talib, Jabal Hira. |

(a) Zama ambazo watu wa arabuni na sehemu zingine walikuwa wakiishi kwa kufuata matashi yao kinyume na mwongozo wa Allah (s.w) ni...Ukristo......................

(b) Kabla ya kuitwa Saud Arabia nchi aliyozaliwa Mtume (s.a.w) ilikuwa inajulikana kwa jina la.........Makkah..........................

(c) Mji ulioanzishwa na Nabii Ibrahim (a.s) na familia yake kwa amri ya Allah (s.w) unajulikana kwa jina la ...AL-Ka'abah...............

(d) Kabla ya kuja Uislamu Waarabu na watu wa sehemu zingine duniani walizama katika dini ya ...Ummul - Qura.............................

(e) Kutokana na ukongwe wa nyumba ya kwanza ya ibada iliyojengwa na nabii Ibrahiim (a.s) nyumba hiyo imeitwa kwa jina la .........Jeddah..............

(f) Mwanzo wa kukua kwa mji wa Bakkah kwa kiasi kikubwa kulichangiwa na kuwepo kwa ....Abu taLib...........

(g) Mji wa Makkah umekuwa mtukufu kwa sababu ya ...Hijaz...........................

(h) Kutokana na utukufu wake Mji wa Makkah umeitwa katika Qur'an kwa jina la ...Baytul Maqdis.....

(i) Uelekeo (kibla) wa kwanza wa ibada za Waislamu ulikuwa ...Baytul Atiq.......

(j) Kiongozi wa kwanza wa mji wa Makkah ambae ni katika mababu wa Mtume (s.a.w) ni ...Jahiliyyah............

Kielelezo Na. 4.2. Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 4

### 2.2.3 Swali la 5: Qur'an

Swali hili lilitoka katika mada ya Qur'an na lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b). Kipengele (a) kilikuwa na muhtasari wa historia ya kushuka kwa Qur'an na kipengele (b) kilikuwa na aya tano za mwanzo za Suratul Alaq (96:1-5). Mwanafunzi alitakiwa kupanga katika mtiririko sahihi katika vipengele vyote viwili. Kila kipengele kilikuwa na alama (5). Hivyo swali lote lilikuwa na jumla ya alama kumi (10). Swali hili lilipima umahiri wa wanafunzi kuelewa historia ya Quran na kujua tafsiri yake. Swali lilikuwa kama ifuatavyo;

5. (a) Pangilia muhtasari wa historia ya kushuka Qur'an katika mtiririko wenye kuleta mantiki. Andika namba ya sentensi katika jedwali.

(i) Akiwa pangoni Hira katika mlima Nur usiku wa mwezi wa Ramadhani Allah akamletea aya tano za Surat Alaq.

(ii) Safari hii ndefu iliyochukua miaka 23 ikahitimishwa katika Hijjatul Wada'i pale Allah (s.w) alipotubainishia wahyi wake katika aya tatu za Surat Maida.

(iii) Muda mrefu katika maisha yake alikuwa akijitenga na kutafakari hali ya jamii inayomzunguka.

(iv) Alikuwa na umri wa miaka 40 wakati Allah (s.w) alipomaliza kumuandaa ki-ilhamu Mtume wetu (s.a.w)

(v) Katika hali hiyo Allah (s.w) akamtuma Malaika Jibril (a.s) kwenda kumuonesha nini anapaswa kufanya ili kuunusuru ummah.

(b) Panga katika mtiririko sahihi maamrisho ya Allah (s.w) kwa Mtume (s.a.w) na Waislamu kwa ujumla juu ya kutafuta elimu mbalimbali: Andika namba ya sentensi katika jedwali.

(i) Aliyemuumba mwanadamu kwa pande la damu.


(ii) Amemfundisha mwanadamu mambo mengi aliyokuwa hayajui.

(iii) Soma na Mola wako ni mkarimu mno.

(iv) Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba.

(v) Ambaye amemfundisha mwanadamu kwa kalamu.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi wote 85,565 (100%) waliofanya upimaji. Kati yao, wanafunzi 45,519 (53.20%) walipata alama 3 hadi 6 ambazo ni ufaulu wa wastani. Wanafunzi 24,549 (28.69%) walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2 na wanafunzi 15,498 (18.11%) walipata alama 7 hadi 10 ambazo ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao umeoneshwa katika Chati Na. 5.




**Chati Na. 5** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 5*

Chati Na. 5 inaonesha ufaulu mzuri katika swali hili kwa kuwa kati ya wanafunzi wote waliofanya upimaji huu asilimia 71.31 waliweza kujibu kwa usahihi dhidi ya asilimia 28.69 walioshindwa.

Aidha, wanafunzi waliopata alama za juu katika swali hili walionesha kuwa na ufahamu wakutosha kuhusu historia ya kushuka na kuhifadhiwa Qur'an sambamba na tafsiri yake. Hivyo, waliweza kupanga kwa usahihi sentensi zote katika vipengele (a) na (b).

Katika kipengele (a), mwanafunzi alitakiwa kupangilia muhtasari wa historia ya kushuka kwa Qur'an katika mtiririko wenye kuleta mantiki. Usahihi wa muhtasari huu ulizingatia mfululizo wa matukio kabla na baada ya Wahyi kushuka ambapo tukio la kwanza lilikuwa (iv) na la mwisho (ii). Wanafunzi mahiri katika historia ya kushuka kwa Qur'an waliweza kubaini mpangilio huo na kupanga sentensi hizo katika mtiririko wake.

Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki, walichanganya matukio hayo muhimu na kuonesha kukosa maarifa ya kutosha katika historia ya Qur'an. Baadhi ya wanafunzi walishindwa kufuata malelekezo ya swali badala ya kuandika majibu yao kwa namba za kirumi kwenye jedwali walilopewa wakaandika kwa namba za kiarabu (za kawaida) na wengine walirudia kuandika tena nukuu walizopewa na wachache waliandika herufi.

Kipengele cha (b), mwanafunzi alitakiwa kupanga mtiririko sahihi maamrisho ya Allah (SW) kwa Mtume (SAW) na Waislamu kwa ujumla yanayohusu kutafuta elimu mbalimbali. Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kukumbuka tafsiri ya aya tano za mwanzo za Surat Alaq (96: 1 – 5). Mpangilio sahihi wa aya huwa haufuati maoni ya watu au mantiki ndio maana mwanafunzi alitakiwa kupanga kwa usahihi (kama ilivyopangwa kwenye Qur'an yenyewe). Wanafunzi mahiri katika tafsiri ya Qur'an waliweza kupanga aya hizo kwa usahihi kwa kuwa waliweza kusoma Qur'an na kukumbuka vema tafsiri yake.

Aidha, wanafunzi walioshindwa kupanga kwa usahihi walichanganya aya hizo katika asili yake na kuunda habari zao ambazo ni tofauti na Qur'an. Wanafunzi hao walionesha kutokuwa na maarifa yakutosha katika usomaji na tafsiri ya Qur'an. Baadhi ya wanafunzi walishindwa kufuata malelekezo ya swali badala ya kuandika majibu yao kwa namba za kirumi kwenye jedwali walilopewa wakaandika kwa namba za kiarabu (za kawaida) na wengine walirudia kuandika tena nukuu walizopewa na wachache waliandika herufi.

Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kupanga kwa usahihi nukuu hizo katika vipengele vyote viwili na Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kupanga nukuu hizo kwa usahihi katika vipengele vyote.


(a)

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| iv | iii | v | i | ii |

(b)

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| iv | i | iii | v | ii |

Kielelezo Na. 5.1 Sampuli ya Majibu Sahihi ya Wanafunzi katika Swali la 5




Kielelezo Na. 5.2. Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 5


## 2.3 Sehemu C: Majibu Mafupi na Insha

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (6 na 7) ambapo kila moja lilikuwa na alama 20 hivyo jumla ya alama katika sehemu hii ilikuwa 40. Maswali yote mawili yalitoka katika mada za Fiqh na mwanafunzi alitakiwa kujibu maswali yote.

### 2.3.1 Swali la 6: Fiqh kwa Ujumla

Swali lilikuwa na vipengele vitano (a) hadi (e) ambapo mwanafunzi alitakiwa kujibu vipengele vyote kwa ufupi. Vipengele vilivyounda swali vilitoka katika mada ndogo zifutazo; *Dhana ya nguzo za Uislamu, Shahada, Kusimamisha Sala, Kutoa Zakat na Kufunga mwezi wa Ramadhani*. Kila kipengele katika swali hili kilikuwa na alama nne (04) hivyo swali lote lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali lilijibiwa na wanafunzi wote 85,565 (100%) waliofanya upimaji huu, ambapo kati yao wanafunzi 74,127 (86.63%) walipata alama 0 hadi 4 ambazo ni dhaifu. Wanafunzi 10,790 (12.61%) walipata alama 5 hadi 12 ambazo ni wastani na wanafunzi 648 (0.76%) walipata alama 13 hadi 20 ambao ni ufaulu mzuri. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao umeoneshwa katika Chati Na. 6.




**Chati Na. 6** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 6*


Chati Na. 6 inaonesha ufaulu hafifu katika swali hili kwa kuwa kati ya wanafunzi wote waliofanya upimaji huu ni asilimia 13.37 pekee ndio waliweza kujibu kwa usahihi dhidi ya asilimia 86.63 walioshindwa.

Aidha, ufaulu hafifu katika swali hili ulichangiwa na wanafunzi kukosa maarifa ya kutosha katika mada mbalimbali za Fiqh kama ilivyobainishwa katika uchambuzi wa majibu ya wanafunzi hao katika kila kipengele:

Katika kipengele (a) mwanafunzi alitakiwa kueleza kwa ufupi maana ya kauli ya Mtume (SAW) aliposema "Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano". Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima wanafunzi umahiri wa kuchambua dhana ya Uislamu kujengwa juu ya nguzo tano ili kuondoa ufahamu usio sahihi ulioenea katika jamii juu ya nguzo za Uislamu.

Wanafunzi mahiri katika dhana ya nguzo za Uislamu waliweza kutambua vema matakwa ya swali na kueleza kwa muhtasari maana ya kauli hiyo ya Mtume (SAW). Baadhi ya wanafunzi hao walieleza kuwa: *"Uislamu wa mtu haukamiliki ispokuwa kwa kutekeleza nguzo tano, yaani ili uislamu wa mtu ukamilike anatakiwa kuzitekeleza nguzo zote za uislamu kwa ukamilifu kama ilivyofafanuliwa na sharia pamoja na kufanya mambo mengine yaliyoamrishwa na Allah (s.w) na kuacha makatazo yote."* Wengine waliandika *Nguzo za Uislamu ni nyenzo katika kuliendea lengo la maisha ambalo ni kumuabudu Mwenyezi Mungu katika maisha yetu yote, hivyo*

*nguzo hizo ni njia kuelekea malengo lakini sio malengo yenyewe.* Wanafunzi hawa walielewa vema kuwa nguzo za Uislamu ni nyenzo katika kuutekeleza Uislamu na sio mwisho wa Uislamu wenyewe. Kielelezo Na 6.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 6(a).


(a) "Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano." Nini maana ya kauli hiyo ya Mtume (s.a.w)?


- Kauli hii ya mtume inayosema "Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano", inamaanisha kuwa uislamu wa mtu haukamiliki isipokuwa kwa kutekeleza nguzo tano. Yaani ili uislamu wa mtu ukamilike, mtu anatakiwa kutekeleza nguzo zote za uislamu kwa ukamilifu kama ilivyo fafanuliwa na sheria pamoja na kufanya mambo mengine yaliyoamrishwa na Allah (s.w) na kuacha makatazo yote.

Kielelezo Na. 6.1 Sampuli ya Majibu Sahihi ya Wanafunzi katika Swali la 6(a)

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, majibu yao yalitofautiana kwa sababu mabalimbali. Baadhi yao walionesha kutoelewa matakwa ya swali na kujibu hoja ambazo hawakuulizwa kama vile kuorodhesha nguzo tano za Uislamu, kutaja nguzo ya Ihsan na Imani. Pia, wapo walioshindwa kujibu kabisa na kuacha kipengele hiki bila kujazwa. Wengine walionesha kutokuwa na maarifa na kujibu kwa mtazamo potofu wa kijamii, kama vile Uislamu ni kutekeleza nguzo tano tu, na wengine walijibu kuwa: "*Uislamu ni dini ambayo inafuatwa kwa nguzo tano, nguzo hizo ni shahada mbili, kusimamisha swala, kutoa zakat, kufunga swaumu, kuhiji kwa mwenye uwezo ndio maana ya kujengwa uislamu juu ya nguzo tano",* mwanafunzi mwingine aliandika; "*Hizo nguzo ukizifuata wewe unakuwa muislamu wa kweli.".* Majibu haya yalionesha kuwa wanafunzi hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana ya nguzo za Uislamu.

Wanafunzi wengine walijibu kuwa: "*ili muumini wa dini ya kiislamu awe muumini wa kweli lazima atekeleze nguzo zote tano za Uislamu".* Jibu hili sio sahihi kwa sababu kuna baadhi ya nguzo katika hizo zinatekelezwa na watu maalumu, kama vile Zakat na Hijjah nguzo hizi ni kwa wenye uwezo wa mali ama wale wasiokidhi vigezo hawalazimiki kutekeleza, hata hivyo

bado wanabaki kuwa waumini. Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 6(a).




(a) "Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano." Nini maana ya kauli hiyo ya Mtume (s.a.w)?

Uislamu ni dini ambayo imaguatwa kwa nguzo tano nguzo hizo ni, Shahada mbili, kusimamisha swala, kutoa zakat, kufunga swaum, kuhijib kwa mwenye uwezo ndiyo maana ya kujengwa uislamu juu ya nguzo tano.

Kielelezo Na. 6.2 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 6(a)

Katika kipengele cha 6 (b) mwanafunzi alitakiwa ataje malengo au makusudio ya kutekeleza nguzo nne kati ya nguzo tano za Uislamu alizopewa katika katika vipengele vidogo vinne (i – iv). Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima wanafunzi umahiri wa kuelewa kazi kuu ya nguzo hizo ambazo Waislamu wamewajibishwa kuzitekeleza.

Kipengele kidogo cha 6 (b) (i), mwanafunzi alitakiwa kutaja makusudio ya kutamka Shahada mbili. Wanafunzi mahiri katika nguzo ya kwanza ya Uislamu waliweza kutaja kwa usahihi malengo yake kuwa; Shahada imekusudiwa *kuweka ahadi mbele ya Allah (SW) juu ya kutekeleza aliyoyaamrisha…."* Mwanafunzi huyu alielewa vema kwamba Shahada ni kiapo cha utii kwa mwanadamu kuwa hatomtumikia yeyote ila Allah (SW) pekee. Kielelezo Na 6.3 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya wanafunzi katika kipengele cha 6(b) kipengele kidogo cha (i).



(b) Taja makusudio ya kutekeleza nguzo zifuatazo za Uislamu:


(i) Kutamka Shahada mbili.

Makusudio ya kutamka shahada mbili ni kuweka ahadi mbele ya Allah (s.w) juu ya kutekeleza aliyoyaamrisha na kukubali kuwa hapana mola apasaye kuabudiwa kwa hakki isipokuwa ni yeye Allah (s.w). Pia shahada mbili ni kitambulisho cha muislamu katika Ummah wa kiislamu.

Kielelezo Na. 6.3 Sampuli ya Majibu Sahihi ya Wanafunzi katika Swali la 6(b)(i)

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki, baadhi yao walitoa maana ya Shahada kama vile: *Nakubali kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na Muhammad ni Mtume wake*" wengine waliandika *"Mwenyezi Mungu ni mmoja na wala hana mshirika".* Kundi lingine walitoa malengo yasiyo husiana na Shahada, kama vile; *kumfanya mja awe na imani juu ya kile anachokiamini na awe mkweli kwa kila jambo.* Majibu haya hayakuwa mahususi kwa Shahada kwani watu wanaweza kupata imani katika nguzo zingine pia hoja haijabainisha kuhusu imani hiyo ni *juu ya kile anachokiamini* ambacho hajakitaja hivyo majibu haya hayakujitosheleza.

Wengine walijibu; "*Kumfanya muislamu awe mchamungu na kutekeleza maamrisho yake".* Sentensi hakubainisha maamrisho ya nani pia mja kuwa mchamungu ni lengo mahususi la nguzo ya nne ya Uislamu ambayo ni kufunga Ramadhani. Kwa ujumla baadhi ya majibu yalionesha kuwa wanafunzi walielewa matakwa ya swali lakini hawakuwa na maarifa ya kutosha kuweza kujibu kwa usahihi. Wanafunzi wengine walitaja matumizi ya Shahada badala ya kutaja malengo yake, nao waliandika kuwa; "*Mtu anapobadili dini anatamka shahada".* Hawa walionesha kutoelewa matakwa ya swali. Kielelezo Na 6.4 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 6 (b) kipengele kidogo cha (i).


(i) **Kutamka Shahada mbili.**
Ni nguzo ambayo inamfundisha mwanadam
u kutamka shahada mbili pale anapofari
ki au pale anapobadili dini na kuwa mu
islamu ndipo anatakiwa kutamka shahada
mbili.

Kielelezo Na. 6.4 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 6 (b) (i)

Katika kielelezo Na. 6.4 mwanafunzi ameeleza matumizi ya Shahada badala ya kutaja malengo au makusudio yake.

Kipengele cha 6(b)(ii), mwanafunzi alitakiwa kutaja makusudio ya kusimamisha Swala. Wanafunzi mahiri katika nguzo ya pili ya Uislamu

waliweza kubainisha lengo hilo na kujibu kuwa “*Swala imekusudiwa kumkataza mja na mambo maovu na machafu”* wanafunzi hawa walielewa kuwa Swala ni kinga kwa muumini dhidi ya mambo maouvu na machafu. Kielelezo Na 6.5 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 6(b) kipengele kidogo cha (ii).


(ii) **Kusimamisha Swala.**

Lengo la kusimamsha swala ni kumuepusha mja na mambo maovu na machafu kwa kuyaacha mambo yote ambayo Allah(s.w) ameyakataza na kuyafanya yale ambayo Allah (s.w) ameyaamrisha yafanyike.

Kielelezo Na. 6.5 Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6 (b) (ii)

Baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi hawakuelewa matakwa ya swali, wengine hawakuwa na maarifa ya kutosha katika nguzo ya pili ya Uislamu. Miongoni mwa ambao hawakuelewa matakwa ya swali walijibu kuwa; “*Ni kuswali swala tano ambazo mwenyezi Mungu ameziamrisha*.” Mwanafunzi huyu alitoa maana ya kusimamisha Swala badala ya kutaja malengo ya kusimamisha ibada hiyo, majibu hayo yanaonesha kuwa mwanafunzi hakuelewa matakwa ya swali.


Wengine walijibu kuwa; “*Ni kumuwezesha mja kuwa anakaa kwa muda anamkumbuka Allah (s.w) kwa kusali na kumtaja”*. Jibu hili linaonesha kutokuwa na maarifa juu ya nguzo za Uislamu kwa ujumla, kwani Allah (SW) ameweka ishara nyingi katika maisha ya wanadamu ambazo zinasababisha kukumbukwa kwake kila dakika. Wengine katika kundi hili walijibu kuwa; *Kumfanya mja kutambua kuwa ndio nguzo kuu itakayompeleka peponi*”. Zaidi ni kuwa, hawa wamejibu kwa mtazamo potofu kuhusu ibada hii kwamba Swala ya mtu ndiyo itakayompeleka peponi na siyo kubadilika kwa kujiepusha na vitendo viovu na vichafu. Kielelezo Na. 6.6 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 6(b) kipengele kidogo cha (ii).


(ii) Kusimamisha Swala.
Makusudio ya kusimamisha swala katika uislamu ni kudhihirisha kuwa umemwamini, kumnyenyekea Allah (s.w) kwani ni Ibada ambayo Allah (s.w) ameiamrisha itekelezwe pia ni moja wapo ya nguzo ya uislamu.

Kielelezo Na. 6.6 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 6 (b) (ii)

Katika kielelezo Na. 6.6 mwanafunzi ameeleza kusimamisha Swala kama ishara ya imani na utii lengo ambalo ni la jumla katika kutekeleza ibada zote. Jibu hili lilionesha kuwa mwanafunzi hakuwa na maarifa juu ya nguzo ya pili ya Uislamu hivyo alishindwa kutaja malengo au makusudio mahususi ya kusimamisha Swala.

Kipengele cha 6(b)(iii), katika kipengele hiki mwanafunzi alitakiwa kutaja makusudio ya kutoa Zakat. Wanafunzi mahiri katika nguzo ya tatu ya Uislamu waliweza kubainisha lengo hilo kuwa ni *Kutakasa mali na nafsi ya mtoaji na mpokeaji*. Wanfunzi hao walielewa kuwa Zakat ni ibada inayomuathiri mtekelezaji, mpokeaji na jamii kwa ujumla. Kielelezo Na 6.7 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 6(b) kipengele kidogo cha (iii).



(iii) Kutoa Zakat.
Makusudio ya kutoa zakat ni kutakasa na kutukuza jamii – kutokana na madhambi yanayosababishwa na umiliki wa mali katika jamii.

Kielelezo Na 6.7 Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6 (b) (iii)

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki walitofautiana katika makosa yao. Baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na maarifa juu ya nguzo tatu ya Uislamu. Miongoni mwa ambao hawakuelewa matakwa ya swali walitoa maana ya Zakat badala ya kutaja makusudio yake, wanafunzi hawa walijibu kama

ifuatavyo; *Mali anayoitoa tajiri 2.5 au* $\frac{1}{40}$ *kwa kutekeleza amri ya Allah (s.w) baada ya kupinduka mwaka au mavuno iwapo mali yake itafikia nisabu".* Maelezo haya yanatoa maana (taarifu) ya Zakat lakini hayaelezi makusudio ya kutekelezwa kwake, kama ambavyo hoja ya swali imekusudiwa. Wengine walijibu kuwa "*Ni hali ya mtu mwenye uwezo kujitolea kuwalisha masikini ambao hawajiwezi.*" Maelezo ambayo haya yanatoa maana ya Sadaka kwani Zakat ni lazima na kuna viwango mahususi sio kujitolea tu.

Pia, miongoni mwa walioshindwa kujibu vizuri katika kipengele hiki walitaja makundi ya wanaostahiki kupewa Zakat na kuchanganya na dhana ya Sadaka, badala ya kutaja malengo ya kutoa Zakat. Majibu yao yalikuwa kama ifuatavyo:- *ni kumpa mtuambaye hajiwezi masikini au fukara au huduma inayotolewa na mtu maalumu*". Maelezo haya ya mwanafunzi yanataja makundi ya wanaostahiki kupewa Zakat kama vile Masikini na Mafukara na mwisho yanaeleza sifa ya Sadaka ambayo ni huduma inayotolewa na mtu. Kielelezo Na 6.8 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 6(b) kipengele kidogo cha (iii).



(iii) Kutoa Zakat.
Ni jambo analofanya mtu kwa kutoa kiwango kidogo cha mali alichonacho ili kusaidia baadhi ya watu ambao masikini au kujenga msikiti na jambo hili hufanywa na mtu mwenye uwezo mkubwa au mwenye mali ya halali.

Kielelezo Na. 6.8 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 6 (b) (iii)

Katika kielelezo Na. 6.8 mwanafunzi ameeleza maana ya Sadaka badala ya makusudio ya kutekeleza ibada ya Zakat. Jibu hili lilionesha kuwa mwanafunzi hakuelewa matakwa ya swali na hakuwa na maarifa ya kutosha ili kutofautisha baina ya dhana hizo mbili (dhana ya Zakat na Sadaka).

Kipengele cha 6 (b) (iv), mwanafunzi alitakiwa ataje kusudio la kufunga mwezi wa Ramdhani. Aidha, wanafunzi mahiri katika nguzo ya nne ya

Uislamu waliweza kujibu kipengele hiki kwa usahihi kwa kutaja kuwa; *ili kumuandaa mja kuwa Mcha-Mungu*. Wanafunzi hawa walielewa kuwa ibada hii imeamrishwa kwa waumini ili iwe chuo cha mafunzo ya tabia njema na kujikaribisha kwa Mwenyezi-Mungu. Kielelezo Na 6.9 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 6(b) kipengele kidogo cha (iv).


(iv) **Kufunga Mwezi wa Ramadhani.**
Lengo la kufunga mwezi wa Ramadhani ni kumuandaa mja kuwa mchamungo.

Kielelezo Na 6.9 Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6 (b) (iv)

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hili walitofautiana katika makosa yao. Baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na maarifa juu ya nguzo ya nne ya Uislamu. Katika walioshindwa kubaini matakwa ya swali, walijibu kwa kutoa maana ya kufunga kama vile: "*ni kujizuia na kula au kunywa kuanzia alfajiri mpaka magharibi katika mwezi wa Ramadhani.* Maelezo haya ya mwanafunzi yanatoa maana (taarifu) ya kufunga wakati alitakiwa kutaja lengo la funga ambalo ni kumuwezesha mja kuwa mcha-Mungu.

Aidha, wanafunzi waliokosa maarifa katika nguzo ya nne ya Uislamu waliandika majibu yasiyo sahihi kama vile; *Kufunga kwa waislamu ni kutupima imani zetu na kujizuia na kula,* wengine *Kufanya au kuyakumbuka mambo yote aliyokuwa anayafanya mjumbe wa Mwenyezi Mungu au Mtume (SAW)*". Majibu haya yalionesha kuwa wanafunzi hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya Funga. Kielelezo Na 6.10 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya wanafunzi katika kipengele cha 6(b) kipengele kidogo cha (iv).

(iv) Kufunga Mwezi wa Ramadhani.

kufunga Mwezi mtukufu wa Ramadhani kwa ajiri ya kutubu madambi yako na kumrejea mwenyezimungu kwa yote uliyo yatenda katika mwezi wa kawaida.

Kielelezo Na. 6.10 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 6 (b) (iv)

Katika kipengele cha 6(c) mwanafunzi alitakiwa kueleza aina mbili za Sujuud zinazotekelezwa katika kukamilisha ibada ya Swala. Swali lilikuwa na vipengele vidogo viwili (i) na (ii) na lilipima uwezo wa mwanafunzi kuchambua vitendo muhimu katika ibada ya Swala na namna ya kuvitekeleza.

Kipengele 6(c)(i) mwanafunzi alitakiwa kueleze dhana ya Sijdatul Sah-wi, ambapo wanafunzi mahiri katika nguzo ya pili ya Uislamu waliweza kueleza dhana hii kwa ufasaha. Wanafunzi hawa walieleza kuwa Sijdatul sahwi ni: *Sijda ambayo mtu anaileta (anasujudu) baada ya kugundua kuwa amesahau kitendo fulani katika Swala yake*. Wanafunzi walielewa kuwa sijida hii inaletwa ili kukamilisha sehemu iliyosahaulika baada ya kurejea ikiwa sehemu hiyo ni nguzo au bila kurejea kitendo ikiwa mtu atakumbushwa kwa kitendo cha Sunnah. Kielelezo Na 6.11 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya wanafunzi katika kipengele cha 6(c) kipengele kidogo cha (i).

(i) Sijidat Sah-wi


Ni sijida mbili anazozileta mwenye kuswali ili kufidia kitendo cha sunnah alichokisahau baada ya tashahud ya mwisho na kabla ya salam.

Kielelezo Na. 6.11 Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6 (c) (i)

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki, walionesha kutokuwa na maarifa kuhusu Fiqh ya Swala kwa ujumla. Hivyo, baadhi yao walitoa maoni kwa namna walivyofikiri na wengine walieleza mambo

ambayo hayakuulizwa kwenye swali. Miongoni mwa majibu hayo ni kama vile: *Ni dhana ya Allah (s.w) katika fiqhi ya Swala* wengine, *Hii ni Sijida ya kwanza katika rakaa mbili ambayo mtu hukaa itidali na kuomba dua.* Majibu haya hayana asili katika somo hili kwa ujumla hivyo ni wazi kuwa mwanafunzi huyu hakuwa na maarifa yoyote kuhusu Fiqh ya Swala.

Wengine walijibu kuwa; *Ndio kitendo cha kusujudu* majibu ambayo hayana muungano na swali lililoulizwa. Na wengine walijibu kwamba: *ni kitendo cha kuweka paji la uso ardhini".* Majibu haya yanaonesha kuwa wanafunzi hawakuwa na maarifa juu ya dhana hizo. Isitoshe, wengine walichanganya dhana ya Faradh Ain ambayo ni lazima kuitekelezwa na kila Muislamu na dhana ya Sijdatul Sahwi. Kielelezo Na. 6.12 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya wanafunzi katika kipengele cha 6 (c) (i).



(i) Sijidat Sah-wi

Ni mtu ambae amesali alafu Sijidat ikatokea kwenye paji la uso hii ndio inaitwa Sijidat Sah-wi

Kielelezo Na. 6.12 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 6 (c) (i)

Kielelezo Na. 6.12, mwanafunzi ameeleza Sijdat Sah-wi kama athari inayopatikana katika paji la uso baada ya mtu kudumu katika ibada ya Swala kwa muda mrefu.

Katika kipengele 6 (c) (ii) mwanafunzi alitakiwa kueleza dhana ya Sijdatul tilawat. Wanafunzi mahiri katika Fiqh ya Swala waliweza kueleza kwa ufasaha juu ya dhana hii. Wanafunzi hao walieleza yafuatayo katika majibu yao; *Ni Sijda ambayo mtu anaileta wakati Qur'an ikisomwa hususani katika aya zinazosisitiza kusujudu.* Wanafunzi hao walielewa kuwa sijida hii ni ishara ya unyenyekevu na mazingatio juu ya amri za Mwenyezi-Mungu hivyo, katika hali yoyote ile iwe katika Swala au nje ya Swala ni muhimu kuileta pale unapokutana na msisitizo huo katika Qur'an. Kielelezo Na 6.13 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya wanafunzi katika kipengele cha 6 (c) kipengele kidogo cha (ii).




(ii) Sijidat Tilawat

Ni sijda moja anayoileta mwenye kusikiliza au kusoma Qur-an baada ya kutajwa aya ya sijda.

Kielelezo Na 6.13 Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6 (c) (ii)

Aidha, baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi dhana hii, walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu Fiqh ya Swala. Majibu ya wanafunzi hawa yalitofautiana kati ya mmoja na mwingine. Baadhi walijibu kuwa; *Ni aina ya sijda ambayo haifuatwi katika Swala.* Wengine walijibu kama; *Ni aina ya sijda ambayo inahusiana na elimu.* Majibu waliyoyatoa hayakuhusiana na jambo lolote la msingi katika dhana hiyo. Wengine walieleza kama *Ni alama inayojitokeza kutokana na kusali kwa muda mrefu katika maisha*. Wanafunzi hao walidhani kuwa Sijida ni athari inayopatikana katika paji la uso au magotini na si kitendo. Hali hii inaonesha kuwa hawakuwa na maarifa kuhusu Fiqh ya Swala. Kielelezo Na. 6.14 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 6(c) kipengele kidogo cha (ii).



(ii) Sijidat Tilawat

Ni mtu ambae amaswali kwamudo mrefu alafu baadae Sijidat ikatokea kwenye magoti hiyo ndio inaitwa Sijidat tilawat.

Kielelezo Na. 6.14 Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 6(c)(ii).

Kielelezo Na. 6.14 mwanafunzi ameeleza Sijdat Tilawat kama athari inayopatikana katika magoti baada ya mtu kudumu katika ibada ya Swala kwa muda mrefu.

Katika kipengele cha 6 (d) mwanafunzi alitakiwa kutaja kiwango cha Nisaab katika aina nne za mali alizopewa katika vipengele vidogo vinne (i) hadi (iv). Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kukumbuka viwango na aina za mali zinazofaa kutolewa Zakat ambayo ni nguzo ya nne ya Uislamu.


Katika kipengele 6 (d) (i) mwanafunzi alitakiwa kutaja kiwango cha Nisaab ya mali ya kuokota. Wanafunzi mahiri katika Zakat walitaja kuwa mali ya kuokota *Haina kiwango maalumu.* Wanafunzi hao walielewa kuwa mali ya kuokota ya kiwango chochote inapaswa kutolewa Zakat. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu walitaja viwango mbalimbali na wengine kujibu kuwa haitolewai Zakat. Wanafunzi hao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kipengele hiki na kujibu kwa maoni yao binafsi.

Kipengele cha 6 (d) (ii) mwanafunzi alitakiwa kutaja kiwango cha Nisaab ya Mbuzi. Wanafunzi mahiri katika Zakat walitaja kuwa Nisaab ya Mbuzi ni *Arobaini (40)* Wanafunzi hao walielewa kuwa Mbuzi anawekwa kundi moja na Kondoo, ambapo ikiwa mmiliki atafikisha 40 atalazimika kutoa Zakat. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu walitaja viwango mbalimbali kama vile mbuzi mmoja, nusu ya yake. Wanafunzi hao walionesha kutoelewa vema dhana ya Nisaab kwani wengi walitaja viwango vya kutoa na si kima cha chini cha utoaji.

Kipengele cha 6 (d) (iii), mwanafunzi alitakiwa kutaja Nisaab ya Dhahabu na Vito, ambapo katika kipengele hiki wanafunzi wote waliofanya upimaji huu walishindwa kujibu kwa usahihi. Wanafunzi wengi walitaja viwango mbalimbali kutokana na maoni yao na wengine waliacha kujibu kabisa. Aidha, Nisaab ya *Dhahabu na vito* ni Gram 82.5 au Tola 7.5.


Kipengele cha 6 (d) (iv), mwanafunzi alitakiwa kutaja Nisaab ya Punda, ambapo wanafunzi mahiri katika Zakat walijibu kuwa Punda hatolewi Zakat. Wanafunzi hao walielewa kuwa mnyama Punda si katika aina za mali zinazopaswa kutolewa Zakat. Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu walitaja idadi mbalimbali na wengine kujibu kwa mbadala k.v Mbuzi mmoja na wengine Kondoo.

Kukosekana mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele vyote kwa usahihi ni ishara kuwa wanafunzi wengi hawazingatii mada ya Zakat hususani viwango vya chini vya mali vinavyopswa kutolewa (Nisaab) kwa kuwa elimu ya Zakat haifanyiwi kazi sana katika jamii. Kielelezo Na. 6.15 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vizuri katika swali la 6 (d) na Kielelezo Na. 6.16 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi vipengele vyote.


(d) Bainisha kiwango cha Nisaab cha mali zifuatazo katika utoaji Zakat.
(i) Mali ya kuokota - Haina kiwango maalumu.
(ii) Mbuzi - Mbuzi 40.
(iii) Dhahabu na vito - gramu 52.
(iv) Punda - Punda hatolewi Zakat.

Kielelezo Na. 6.15 Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6 (d)

Kielelezo Na. 6.15 kinaonesha sampuli ya mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi katika vipengele vitatu (i, ii na iv) na kushindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele cha (iii) ambacho majibu yake sahihi ni Gramu 82.5 au Tola 7.5



(d) Bainisha kiwango cha Nisaab cha mali zifuatazo katika utoaji Zakat.
(i) Mali ya kuokota Nusu ya mali
(ii) Mbuzi Kilo mbili na nusu za nyama yake.
(iii) Dhahabu na vito Robo ya vitu hivyo
(iv) Punda Punda mmoja.

Kielelezo Na. 6.16 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 6 (d)

Kielelezo Na. 6.16 kinaonesha majibu ya mwanafunzi ambaye hakuwa na maarifa kuhusu nguzo ya Zakat hususani viwango vya Nisaab na hatimaye kujibu kwa kukadiria viwango hivyo kwa maoni yake.

Katika kipengele (e) mwanafunzi alitakiwa kutoa hoja zinazobainisha sababu za kutukuzwa mwezi wa Ramadhani katika Uislamu. Swali hili lilipima uwezo wa mwanafunzi kutathmini matukio katika ibada ya Funga ya Ramadhani na athari au nafasi zake. Wanafunzi mahiri katika nguzo ya

nne ya Uislamu waliweza kutoa hoja sahihi zilizojibu swali hili. Miongoni mwa hoja hizo ni pamoja na; *Kutekelezwa ndani ya Ramadhani ibada ya Funga ambayo ni nguzo ya nne ya Uislamu, Mwezi wa Ramadhani imeshuka ndani yake Qur'an ambayo ni muongozo kwa watu, Ndani ya Ramadhani kuna usiku wenye cheo (lailatul Qadr)ambao ni bora kuliko miezi 1000.* Wanafunzi hao walielewa kuwa dhana ya utukufu wa mwezi wa Ramadhani imetokana na kuwa na matukio yenye nafasi kubwa katika Dini ya Uislamu ambayo yalitokea ndani yake. Kielelezo Na. 6.17 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika kipengele cha 6(e).


(e) Kwa sababu gani mwezi wa Ramadhani umetukuzwa katika Uislamu? Toa hoja mbili.

(i) - Kwa sababu ndiyo mwezi ambao Qur'an imeshuka ndani yake.


(ii) - Kwa sababu ndiyo mwezi ambao ndani yake kuna usiku wenye cheo (Lailatul Qadir) uliokuwa mtukufu/bora kuliko miezi 1000.

Kielelezo Na 6.17; Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6 (e)

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili baadhi yao walionesha kukosa maarifa kuhusu Funga ya Ramadhani na historia yake, wengine walishindwa kutathmini matukio makubwa katika matukio yaliyojitokeza ndani ya mwezi huo. Baadhi ya wanafunzi hao walitoa hoja zifuatazo; *Kwa sababu ndio mwezi mkubwa kuliko miezi yote ya Kiislamu, Kwasababu unajitokeza kila mwaka mara moja.*Hoja zote mbili hazina mantiki kwani miezi yote ina siku 29 au 30 hivyo hakuna mwezi mkubwa katika Uislamu, lakini pia miezi yote inajitokeza mara moja kwa mwaka, hivyo ni wazi kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu Funga ya Ramadhani.

Wengine walitoa hoja kuwa; *Ni mwezi mtukufu kuliko miezi yote, Ni mwezi wa kumuomba Mwenyezi Mungu, Kwa sababu shetani anakuwa amefungwa minyororo, Kwa sababu ni mwezi wenye neema na baraka, Kwa sababu ni mwezi wa kutubu mazambi.* Hoja nyingi zilizotolewa ni aidha zilikuwa za jumla (sio mahususi) kama vile *kutubu madhambi* hili ni jambo la kila siku si Ramadhani pekee. Hoja nyingine ni matukio ambayo

hayajapewa uzito mkubwa kwa mfano *kufungwa kwa mashetani* pamoja na kuwa ni jambo lililotajwa na Mtume (SAW) lakini halijapewa uzito mkubwa uliosababisha kutukuzwa mwezi huo. Kielelezo Na. 6.18 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya wanafunzi katika kipengele cha 6 (e).


(e) Kwa sababu gani mwezi wa Ramadhani umetukuzwa katika Uislamu? Toa hoja mbili.

(i) kwa sababu ni mwezi wenye neema na baraka tele ndani yake

(ii) kwa sababu ni mwezi wa kutubu mazambi yako na kumrudia mwenyezimungu.


Kielelezo Na. 6.18 Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 6(e).

Kielelezo Na. 6.18 kinaonesha majibu ya mwanafunzi ambayo hayajibu swali la msingi kwani hoja zote zinaeleza mambo yanayopatikana pia katika miezi mingine ya mwaka.

### 2.3.2 Swali la 7: Fiqh ya Swala.

Swali hili lilitoka Fiqh ya Swala ambapo mwanafunzi alitakiwa kufafanua sifa tano za mavazi yanayokubalika kisheria kwa kijana wa Kiislamu aliye baleghe. Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kutathmini sifa za mavazi bila kujali tofauti za kitamaduni ambalo linalokidhi vigezo vya kisheria vya Kiislamu. Swali lilikuwa la muundo wa insha lenye jumla ya alama 20.

Swali lilijibiwa na wanafunzi wote 85,565 (100%) waliofanya upimaji, kati yao, wanafunzi 48,610 (56.81%) walipata alama 0 hadi 4 ambao ni ufaulu dhaifu. Wanafunzi 27,839 (32.54%) walipata alama za wastani kuanzia 5 hadi 12 na wanafunzi 9116 (10.65%) walipata alama 13 hadi 20 ambazo ni alama za ufaulu mzuri. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa wastani kwakuwa kati ya wanafunzi wote waliofanya upimaji asilimia 43.19 waliweza kupata alama kuanzia 5 hadi 20. Muhtasari wa ufaulu wa wanafunzi hao umeoneshwa katika Chati Na. 7.




**Chati Na. 7:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 6*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika swali la 7 umeonesha kuwa wanafunzi waliojibu kwa usahihi swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Fiqh ya Swala hususani katika masharti ya Swala. Aidha, walielewa vema matakwa ya swali, hivyo waliweza kujibu kwa usahihi.

Miongoni mwa sifa walizobainisha ni pamoja na; *Vazi listiri sehemu zote za mwili ambazo hazipaswi kuonekana, lisiwe lenye kubana na kuonesha ramani za mwili, Liwe zito kiasi cha kutoonesha mwili wake, Linapaswa kuendana na jinsia ya mvaaji kulingana na tamaduni za jamii yake, Lisiwe ni vazi rasmi la ibada linalotumiwa na watu wa Dini nyingine tofauti na Uislamu, Lisiwe la gharama kubwa na kujifaharisha, Lisiwe na mapambo mengi yenye kuvuta hisia za watu (hususani kwa wanawake, liwe vazi safi sio chafu na la kujidhalilisha*. Wanafunzi hawa walielewa kuwa dhana ya mavazi katika Uislamu ni ibada, hivyo ni jambo linalosimamiwa na kanuni na taratibu zilizofundishwa na Mwenyezi-Mungu na Mtume wake. Kielelezo Na 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali hili.

7. **Fafanua sifa tano za mavazi yanayokubalika kwa kijana wa Kiislamu aliye balegh.**

Uislamu, ni dini ambayo imekamilika kwa kila kitu. Katika swala la uvaaji, yapo maelekezo mbalimbali juu ya mavazi ya kiume na mavazi ya kike. Ukizingatia katika stara ya mwanaume, vazi-~~at~~ analotakiwa kuvaa linatakiwa kuanzia kitovuni mpaka chini ya magoti, halikadhalika kwa vazi la mwanamke linatakiwa kufunika mwili mzima isipokuwa uso na viganja vya mikono. Zifuatazo ni sifa za mavazi yanayokubalika kwa kijana wa kiislamu aliyebalegh.

Vazi lisiwe lenye kuonyesha aurah. Kijana wa kiislamu aliyebalegh hatakiwi kuvaa vazi lenye kuonyesha, ambalo linaweza kupelekea kuonyesha maumbo /sehemu za ndani za kijana huyo (aurah). Hii ni kwa sababu ni kosa la jinai kwa kijana wa kiislamu kuonesha aurah hadharani.

Vazi lisiwe la majivuno na kiburi. Kijana wa kiislamu aliyebalegh hatakiwi kuvaa vazi ambalo ni la majivuno na kiburi. Iwapo atafanya au ~~kuvaa~~ atavaa vazi la namna hiyo basi atakuwa mwenye kupotea kwani litampelekea kumuasi Allah (s.w) na kwenda kinyume na maamrisho na makatazo yake.

Vazi lisiwe chafu na kujidhalilisha. Vazi ambalo ni chafu na la kujidhalilisha, halifai kwa kijana wa kiislamu aliyebalegh kwani sifa mojawapo ya muislamu aliyosisitiza mtume (s.a.w) ni usafi wa moyo pamoja na usafi wa kawaida kiujumla (mazingira, mwili na mavazi). Hivyo si vizuri kwa kijana wa kiislamu kuvaa mavazi hayo kwani hushusha ~~t~~ hadhi yake katika jamii.

Vazi lisiwe la kizahari. Kijana wa kiislamu hatakiwi kuvaa vazi la kizahari katika maisha yake anoyoishi katika jamii. Hii ni kwa sababu, vazi hilo linaweza kuwa sababu kubwa kwa kijana huyo kuchupa ~~mik~~ mipaka ya Allah (s.w) na kutenda madhambi ambayo hayastahili kwa kijana huyo.

Vazi lisiwe lenye kubana na kupendezesha mwili. Vazi la kijana wa kiislamu aliyebalegh halipaswi kuwa lenye kubana wala lenye kupendezesha mwili. Ili kuepukana na hilo au ili kufuata misingi bora ya uvaaji, kijana wa kiislamu anatakiwa kuvaa vazi la kawaida na lisilo la kupendeze ili kuepuka kumuasi Allah (s.w).

Hivyo, ni wajibu kwa kila muislamu kutoa elimu juu mambo ambayo ni ya kheri. Pia ni vyema kwa kila muislamu / waislamu kukumbushana kunako mwenendo bora aliousundisha Mtume Muhammad (s.a.w) katika vitu mbalimbali ili kuishi katika utaratibu anaoundhia Allah (s.w) kwa mwanadamu na maisha yake kiujumla hapa Duniani.

Kielelezo Na. 7.1; Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 7

Aidha, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili baadhi yao walionesha kutokuwa na maarifa kuhusu Fiqh ya Swala, wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali na wengine walishindwa kujenga hoja zinazofafanua sifa, ingawa walielewa swali na walikuwa na ufahamu kuhusu masharti ya Swala.

Miongoni mwa wanafunzi walioshindwa kuelewa matakwa ya swali walijibu kama ifuatavyo; *Kanzu, Kofia, Baibui, Msuli, Mitandio, Majuba, Nikabu na Mavazi mengine.* Wanafunzi hawa walishindwa kuelewa matakwa ya swali kwani badala ya kueleza sifa za mavazi yanayokubalika wakaeleza aina ya mavazi mbalimbali.


Wanafunzi wengine walitoa hoja moja tu na kuieleza, wanafunzi hawa walijibu kuwa sifa ya vazi la kijana ni *Stara*. Wanafunzi hao walishindwa kujenga hoja ya kujibu swali hili kwa ukamilifu ingawa walielewa matakwa yake. Jambo ambalo hawakuelewa ni kuwa, *Stara* ni sifa ya jumla inayokamilishwa na vipengele vidogo kadhaa hivyo stara inasimama kama matokeo ya kukamilishwa kwa sifa angalau tano zilizobainisha hapo awali.

Wengine katika walioshindwa kuelewa matakwa ya swali walieleza faida za mavazi ya stara badala ya sifa za mavazi hayo, kundi hili walieleza yafuatayo; *Kuheshimiwa, Kuepuka vishawishi, Kupendwa na jamii, Kuepuka makundi hatarishi na mifano mingine kama hiyo*. Majibu ya wanafunzi hawa yalidhihirisha kuwa hawakubaini matakwa ya swali hili hivyo walishindwa kupata alama nzuri katika swali hili na wengine kupata sifuri.

Wapo wanafunzi walifafanua sifa za mavazi ya kiislamu kwa upande mmoja tu wa jinsia ya kiume au ya kike kinyume na matakwa ya swali ambalo lilimtaka mwanafunzi aeleze sifa za mavazi kwa ujumla kwa jinsia zote. Hoja hizi zinathibitisha kuwa wanafunzi hao hawakuelewa matakwa ya swali. Hivyo hawakujibu swali kama lilivyotakiwa na ikapelekea kutopata alama.

Wanafunzi wengine walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya Fiqh ya swala kwa ujumla. Wanafunzi hao walitoa hoja zifuatazo: *Kuwa tohara kwa mtoto wa kiume, Kuwa muislamu wa kweli, Vazi ni kitendo cha kumpa mtu uhuru*

*katika maisha yake, Vazi ni chanzo cha kuwa na dalili ya kuogopa kuwa mchamungu, Ushauri kwa vazi la kiislamu kujikinga na masheitwani na majini.* Hoja hizi zinaonesha kuwa wanafunzi hao walikosa maarifa ya kutosha kuhusu masharti ya vazi la Kiislamu hivyo walijibu kwa maoni yao. Kielelzo namba 7.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali la 7.



7. **Fafanua sifa tano za mavazi yanayokubalika kwa kijana wa Kiislamu aliye balegh.**

Hijabu; Msichana aliye balegh ame amrishwa na analazimika kuvaa hijabu ili kuustili mwili au kichwa chake kwasababu msichana aliye balegh baadhi ya viungo vyake vya mwili vimekuwa na vinajionesha kwa hiyo anapaswa kuvaa hijabu ili kujistiri.

Kanzu; Ni vazi la heshima ambalo kijana au vijana wa Kiislamu wanapaswa kuvaa na pia ni vazi ambalo walilokuwa wanalitumia mashahaba, mtume na mara bii katika zama zilizopita na ukivaa una vaa vazi hili unatekeleza sunna ~~na unapata~~ za mtume.

Baibui; Ni vazi analopaswa binti au msichana wa Kiislamu kuli vaa kwasababu ni vazi la heshima na lenye kuustiri mwili wako kuanzia juu mpaka chini ambalo vazi hilo unafanya kupunguza matama nio kwa wanaume kwasababu umeuhifadhi mwili.

Nikabu; hii ni vazi lingine ambalo wanawake au mabinti wa Kiislamu wana takiwa kuvaa kwa ajili ya kutoleta mata manio mfano matamanio ya sauti, umbile yaani uso kuufunika unafanya mtu kutouona uso au sura yako na nikabu mafanya sauti yako isikike taratibu;

Wanauma kutovaa vazi la hisbali; Ni vazi ambalo mwanaume atakiwi kuli vaa ni ~~vat~~ kanzu kubuniziKa mpaka chine kama mwanamke haitakiwi ila kuvaa nguo iliyo juu ya ugoko wa miguugu hivyo si ruhusa na unafananishwa na mwanamke.

Mwisho; zilizopo juu ni sifa ya mavazi yaliyoruhusiwa kuvaa kwa kijana wa Kiislamu kuvaa nguo ndefu yenye stara kwa mwana mke na mwana umwe kiji stiri kwa kufuata mipaka yako uliyoonoshwa ushauri tukijistiri kwa wanawake na wanaume tutapunguza matamanio pande zote mbili.

Kielelezo Na. 7.2 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 7

Katika kielelzo namba 7.2 mwanafunzi ameshindwa kubainisha sifa stahiki za mavazi ya kisheria badala yake akafafanua aina za mavazi katika hoja nne na kumalizia na sifa moja mahususi kwa vazi la kiume katika hoja ya tano ambayo ni *kutovaa isbali* (nguo inayovuka vifundo viwili vya miguu.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA

Katika upimaji huu mada zifuatzo zilihusika; *Sunnah na Hadithi*, *Tawhiid*, *Tarekh*, *Qur'an* na *Fiqh*. Uchambuzi wa takwimu za matokeo ya wanafunzi kwa mada umeonesha kiwango kizuri cha ufaulu katika mada za; *Tawhiid (86.96%), Qur'an (71.31%), Sunnah na Hadithi (64.52%).* Aidha mada ambazo zilikuwa na ufaulu wa kiwango cha chini ni *Tarekh (27.40%)* na *Fiqh (28.28%),* ambazo zilipimwa katika maswali ya nne, sita na saba. Mada ya *Sunnah* na *Hadithi* ilipimwa katika swali la kwanza. Mada ya *Tawhiid* ilipimwa katika swali la pili na la tatu. Mwisho swali la tano lilipimwa katika mada ya *Qur'an*.

Wanafunzi walifaulu kwa kiwango kizuri katika mada za Tawhiid, Qur'an na katika mada ya Sunnah na Hadithi. Wanafunzi hawa walifanya vizuri katika mada hizo kwa sababu walielewa vizuri matakwa ya maswali na walikuwa na maarifa ya kutosha yaliyowawezesha kujibu kwa usahihi.

Aidha, wanafunzi walipata alama za chini katika mada za Tarekh na Fiqh kwa sababu mbalimbali kama vile; kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika, kutofuata maelekezo ya swali, kutojua matakwa ya maswali. Wanafunzi wengine walishindwa kuwasilisha majibu yao katika swali lililohitaji kuandikwa kwa muundo wa insha hivyo walipata alama za chini. Muhtasari wa takwimu kwa wastani wa kila mada umeoneshwa kwenye kiambatisho ambapo rangi nyekundu inaonesha kiwango cha chini cha ufaulu na rangi ya kijani inaonesha kiwango kizuri cha ufaulu ikiambatana na namba ya maswali katika mada husika. Aidha, hapakuwepo mada iliyokuwa na ufaulu wa wastani (njano).

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu katika upimaji huu wa kidato cha pili (FTNA 2021) katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni cha wastani kwa asilimia 55.70. Uchambuzi huu umeonesha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa ili kuboresha zaidi kiwango cha kufaulu katika upimaji unaofuata. Changamoto zilizojitokeza kwa wanafunzi katika kujibu maswali ni pamoja na: wanafunzi kutofuata maelekezo ya swali, kushindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza, kuorodhesha majibu kwa namba au herufi kwenye swali linalohitaji kujibiwa kwa muundo wa insha, pia kukosa maarifa katika mada mbalimbali hususani mada za *Tarekh* na *Fiqh*.

Ili kuinua zaidi kiwango cha ufaulu katika upimaji ujao, juhudi za ziada zinahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji katika mada za Tarekh na Fiqh, ili kuwapa wanafunzi maarifa ya kutosha na uwezo wa kujenga hoja. Aidha wanafunzi wanatakiwa kujengewa uwezo wa kuelewa matakwa ya maswali na kuwasilisha maarifa katika namna inayostahili. Walimu wanapaswa kutumia vitabu vya kiada vya somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ili kuwapa wanafunzi maarifa stahiki na kuepuka mitazamo potofu katika somo. Ni muhimu pia kuongeza juhudi katika ufundishaji kwa vitendo na kuwashirikisha wanafunzi katika hatua zote za ujifunzaji ili kuimarisha maarifa yao hususani katika mada za *Tarekh* na *Fiqh.*

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha kufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu wawaongoze wanafunzi kujadili katika vikundi na kurejea muhtasari wa somo na vitabu vya kiada ili kupata maarifa rasmi katika mada

(b) Walimu wawapime wanafunzi kwa maswali ya umahiri zaidi dhidi ya maswali ya kukariri.

(c) Walimu warejee uchambuzi wa muhtasari wa somo ili kuwapa wanafunzi wanachostahiki katika mada zote.

**KIAMBATISHO**

**UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA**

| **Na.** | **Mada** | **Ufaulu wa Kila Swali** | | **Asilimia ya Wanafunzi waliopata wastani wa alama 30 au zaidi** | **Maoni** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Namba ya Swali** | **Asilimia ya Ufaulu** | | |
| 1 | Tawhiid | 3 | 91.63 | 86.96 | Vizuri |
| | | 2 | 82.29 | | |
| 2 | Qur'an | 5 | 71.31 | 71.31 | Vizuri |
| 3 | Sunnah na Hadithi | 1 | 64.52 | 64.52 | Vizuri |
| 4 | Fiqh | 6 | 13.37 | 28.28 | Dhaifu |
| | | 7 | 43.19 | | |
| 5 | Tarekh | 4 | 27.40 | 27.40 | Dhaifu |
| **Wastani wa Jumla wa Ufaulu** | | | | **55.70** | **Wastani** |